SUPA JACKPOT
TZS. 1,074,741,067
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mnyeti** kortini kwa madai ya matumizi mabaya ya madaraka

UKURASA 5


Ngawaiya: Upinzani ni kioo serikali ikitumie sasa kujitazama
Ndivyo Chongolo alivyowapa raha wanachama, wananchi
siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Papa Francis; alamsha dunia inayosahau mateso Sudan Kusini, Congo
VYAMA KUTANDAZA MIKEKA
Viache kulaumu, kulalamika vije na jibu kutumia rasilimali kimaendeleo

UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Februari 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581215
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# UFISADI WA KUTISHA

• **Bunge** labaini mchezo mchafu mamlaka serikali za mitaa, Ubungo, Kigamboni, Iringa zatajwa vinara... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**NYUKI WAVAMIA MAZIKO KIJANA ALIYEUA BINTI**
KUNDI la nyuki limewavamia waombolezaji waliokuwa kwenye mazishi ya mwili wa Erick Kwai (32), aliyeuawa...

UKURASA WA 4
**MWIGULU AKERWA NA WABUNGE KULALAMIKA**
WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akerwa na michango ya...

UKURASA WA 5
**LISSU ASIMULIA MAISHA ALIYOISHI UBELGIJI**
MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesimulia ugumu wa...

## Samia aongeza miezi mitatu ulipaji kodi ya ardhi bila riba

UKURASA 2



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, akionyesha kipimo cha kupimia pombe bandia jana, baada ya kuvikamata mkoani humo. **Picha ndogo:** Kamanda Masejo akionyesha lori likiwa na tela lenye tangi la ujazo wa lita 35,000 za spiriti za kutengenezea pombe hiyo, lililokamatwa likishusha mzigo eneo la King'ori, wilayani Arumeru. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**



## Polisi yanasa shehena ya pombe bandia na bangi kilo 250

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAANIKA NJIA KUVUKA MAKUNDI UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Aliyekuwa Shehe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum (kulia), akifurahia jambo na Kaimu Shehe wa Mkoa huo, Walid Alhad Omar (katikati), baada ya kukabidhiana ofisi, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu Mkuu Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) Al Hajj Nuhu Jabir Mruma. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bunge laibua ufisadi wa kutisha

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imesema uchambuzi katika halmashauri za manispaa nne, umebaini kutokuwapo nidhamu ya ukusanyaji na uvujaji wa mapato huku Sh. milioni 689.260 katika Manispaa ya Ubungo zikiingizwa benki na kutolewa siku moja.

Pia imebaini kuna baadhi ya maeneo miamala hufutwa kabisa au baadhi ya tarakimu hurekebishwa bila idhini ya maofisa masuhuli au bila kuwapo kwa nyaraka za uthibitisho wa uhalali wa marekebisho hayo.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stanslaus Mabula, aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha bungeni jijini Dodoma taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2022.

Alisema uchambuzi wa kamati katika taarifa za ukaguzi maalum uliofanyika katika Manispaa za Ubungo, Kigamboni, Ilemela na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, matokeo yanaonesha bado kuna tatizo la nidhamu ya ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya serikali.

"Changamoto hizi zinapaswa kutafutiwa ufumbuzi wa haraka ili kila senti ya serikali

ilete tija katika kuwahudumia wananchi. Miongoni mwa suluhu ni serikali hususani katika ngazi za sekretarieti za mikoa, kujipanga kikamilifu kwa ajili ya kufanya usimamizi madhubuti na ufuatiliaji wa kina katika shughuli zinazotekelezwa na mamlaka za serikali za mitaa zilizo chini yao.

"Kwa sasa inaonekana kuna ulegevu katika sekretarieti za mikoa katika kuzisimamia halmashauri. Ulegevu huu hautavumiliwa hata kidogo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa," alisema.

Pia alisema kuna uvujaji mkubwa wa mapato ya serikali katika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato wa serikali za mitaa na kwamba endapo mfumo huo utakuwa bado unaendelea kutumika katika baadhi ya halmashauri uvujaji utaendelea.

"Uvujaji huu unasababishwa na baadhi ya watumishi wa serikali wasio waaminifu wanaohusika moja kwa moja na uingizaji wa miamala katika mfumo huo. Ushahidi uliopo unahusiana na Mfumo uliokuwepo awali wa LGRCIS ambao kwa sasa ni TAUSI.

"Kamati ina maoni kwamba kinachofanyika ni wizi kwa sababu ya mazingira ambamo marekebisho ya miamala hufanyika," alisema.

**MANISPAA UBUNGO**

Alisema katika Manispaa ya Ubungo, taarifa ya wadaiwa katika mfumo ilifanyiwa ghiliba kiasi cha kushindwa kuonyesha mapato halisi ya halmashauri kwa kuingiza kiasi cha Sh. 500,666,683,784,266,000,000,000/= ambacho badaye kilifutwa kwa maelezo kwamba kilikosewa.

"Hata hivyo, Manispaa haikutoa maelezo ya kiasi halisi kilichotakiwa kuandikwa kilikuwa ni kipi; Juni 16, 2019 muamala wa Sh. 471,410,886 ulirekebishwa katika mfumo na kuwa Sh. 450, 029, 376 bila ya idhini ya Ofisa Masuuli. Marekebisho haya yanaleta upungufu wa kiasi cha Sh. 21,381,510/= ambazo kamati ina maoni kuwa zimechukuliwa na watumishi waliohusika na marekebisho," alisema.

Pia alisema miamala ya Sh. milioni 156.9 ilirekebishwa kwenye Mfumo wa LGRCIS bila kuwa na nyaraka za kuthibitisha uhalali wa marekebisho hayo.

"Septemba 4, 2019 kiliingizwa kiasi cha Sh. milioni 689.260 katika akaunti ya Manispaa na kutolewa siku hiyo hiyo kama fedha taslimu kwa maelezo kuwa benki (CRDB) ilikosea kwa kuandika namba ya simu ya mteja.

"Kamati ilitaka kujua kiasi halisi ambacho kilitakiwa kuandikwa lakini haikupata maelezo, kamati ndiyo maana ina maoni kuwa huenda palikuwa na vitendo vya utakatishaji wa fedha," alisema.

**MANISPAA KIGAMBONI**

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo ya fedha yaani 2018/2019- 2020/21, watumishi wasio stahili wa Manispaa walifanya marekebisho ya miamala ya mapato ya Sh. 10,857,780,242 bila idhini ya ofisa masuhuli.

Pia alisema maelezo ya Halmashauri hayakuweka bayana sababu za kufanyika kwa marekebisho hayo.

"Ndiyo maana kamati inaona kwamba nyuma ya marekebisho haya huenda kuna nia ovu dhidi ya mapato ya serikali. Jambo hili linahitaji uchunguzi zaidi ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria," alisema.

**ILEMELA IMO**

Kiongozi huyo alisema ukaguzi maalum ulijielekeza katika vipindi vitatu vya miaka ya fedha (2018/19- 2020/21).

"Septemba 30, 2021 CAG alitoa taarifa yenye matokeo ya ukaguzi maalum kwa Manispaa ya Ilemela.

Baada ya zaidi ya mwaka mmoja kupita, yaani Januari 18, 2023 manispaa ilianza kushughulikia hoja za ukaguzi zilizomo kwenye taarifa hiyo ambapo imeweza kujibu hoja tano kati ya 30.

"Baadhi ya hoja za ukaguzi zilizobainika katika Halmashauri ni serikali lazima ichukue hatua za haraka dhidi ya watumishi wote waliohusika,' alisema.

Alisema ankara za Sh. bilioni. 8.7 zilirekebishwa kwenye mfumo wa mapato bila kufuata taratibu na Sh. bilioni 1.4 zilipelekwa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kujenga jengo la wasafiri katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza, bila kuwa na mkataba wa makubaliano juu ya namna ambavyo Manispaa ingenufaika na uwekezaji huo.

"Jumla ya stakabadhi 822 za mapato hazionekani katika daftari la fedha la mfumo wa ukusanyaji wa mapato; Sh. milioni 627.8 hazikupelekwa benki mpaka sasa; hakuna ushahidi wa malipo ya kiasi cha Sh. milioni 356.4 kwamba zililipwa kwa Mhandisi Mshauri Elekezi katika usimamizi wa mradi wa stendi ya mabasi na maegesho ya malori.

"Manispaa ilimlipa mkandarasi aliyejenga hiyo Sh. milioni 237.6 ikiwa ni zaidi ya fedha anazodai. Ilimlipa mkandarasi (TBA) Sh. milioni 138.7 kwa kazi ambazo hajafanya.

Watumishi waliohama na wengine kustaafu wakawa bado wanaingia kwenye Mfumo wa Mapato kiasi cha kutishia usalama wa mfumo wa serikali katika ukusanyaji wa mapato.

"Katika hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha 2019/20 manispaa ili ripoti zaidi madeni ya wazabuni na makandarasi Sh. milioni 200, Sh. milioni 15.6 ikilipwa kwa mkandarasi Ejae Investment Group kwa kutumia risiti ya kughushi hivyo kuikosesha Serikali Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sh.milioni 2.8," alisema.

## Rais Samia aongeza miezi mitatu kulipa kodi ya ardhi bila riba

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza muda wa msamaha wa kulipa kodi ya pango la ardhi bila riba kwa miezi mitatu hadi Aprili 30, mwaka huu.

Aidha, amewataka wananchi ambao wanadaiwa kodi hiyo, kulipa kabla ya muda wa huruma uliotolewa kwisha.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Meandeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya wizara hiyo.

"Natoa rai kwa taasisi na mashirika ya umma na wananchi wote kutumia muda uliotolewa hadi Aprili 30 na Rais Samia kunufaika na msamaha wa riba uliotolewa kulipa deni la msingi ili wasamehewe riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi," alisema.

Waziri Mabula alisema Raisameridhia kuongeza kipindi cha msamaha hadi Aprili, mwaka huu, na uamuzi huo umefikiwa kutokana na sababu mbalimbali za maombi mengi ya wananchi na taasisi kuhusu kuongezewa muda.

Dk. Mabula alisema Rais alitoa msamaha wa riba ya malimbikizo ya pango la ardhi ambapo wananchi wenye malimbikizo walipewa nafuu ya kulipa deni la msingi, ili wasamehewe riba ya malimbikizo kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka jana.

Aliongeza katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka jana, wizara ilikusanya Sh. bilioni 90.9 sawa na asilimia 75 ya lengo la makusanyo ya Sh. bilioni 121.

Kadhalika, alisema makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/23 yameongezeka kwa Sh. bilioni 33.9 ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Aidha, alisema wananchi 6,211 wamenufaika na msamaha wa riba ya malimbikizo ya Sh. bilioni 11.93 hivyo fedha hizo zilizosamehewa zimeenda kuleta nafuu kwa wahusika na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii nchini.

Waziri Mabula pia alisema taasisi na mashirika 73 yanadaiwa Sh. bilioni 63.6 ikiwa ni madeni ya pango ya ardhi.

Mwaka jana Rais Samia aliongeza muda wa miezi mitatu hadi Desemba 31, mwaka 2022.



## HABARI KITAIFA

# Polisi wakamata pombe bandia, bangi kilo 250

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kusafirisha maboksi 154 ya pombe bandia na tangi lenye ujazo wa lita 35,000 lililokuwa na spiriti ya kutengeneza pombe hizo.

Jeshi hilo pia limekamata stika za kampuni mbalimbali za vinywaji pamoja na vifungashio vya pombe.

Pia limekamata dawa za kulevya aina ya bangi magunia matano yenye uzito wa kilo 250 katika oparesheni maalum iliyofanyika Kijiji cha Kisimiri Juu, Arumeru mkoani hapa, iliyokwenda sambamba na kuteketeza ekari saba za dawa hizo haramu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Godfrend Brown (44), mfanyabiashara na Mkazi wa Sanya Juu mkoani Kilimanjaro na Steve Haule (32) dereva wa lori aina ya Scania yenye namba za usajili T. 191 CTB likiwa na tela lake lenye namba za usajili T. 823 DHC ambalo ni tangi lenye ujazo wa lita 35,000 za spiriti.

"Februari 4, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni Jeshi la Polisi tulianza operesheni maalum ya kuwatafuta watu wote wanaojihusisha na utengenezaji wa pombe haramu kwa kutumia nembo za kampuni zilizosajiliwa. Majira ya saa 02:00 eneo la King'ori wilaya ya Arumeru, tulikamata lori hilo likiwa linashusha mzigo wa spiriti kwa lengo la kwenda kutengeneza pombe bandia ambayo ni kinyume cha sheria," alisema.

Kamanda Masejo alisema uchunguzi wa awali wa polisi umebaini kuwa watuhumiwa hao, wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya kihalifu kwa muda mrefu na kufanya biashara hiyo haramu.

"Watuhumiwa bado tunaendelea kuwashikilia kwa ajili ya mahojiano ya kina na upelelezi ukikamilika, jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya kulitolea uamuzi wa kisheria,"alisema.

Kuhusu dawa za kulevya aina ya bangi, Kamanda Masejo alisema Februari 2, mwaka huu, majira ya saa 03:00 asubuhi katika Kijiji cha Kisimiri Juu, Arumeru, polisi walifanya operesheni maalum na kufanikiwa kukamata magunia matano ya dawa za kulevya na kisha kuteketeza ekari saba za mashamba ya bangi.

# Nyuki wavamia maziko kijana aliyeua binti

**Na Jenifer Gilla**

KUNDI la nyuki limewavamia waombolezaji waliokuwa kwenye mazishi ya mwili wa Erick Kwai (32), aliyeuawa na wananchi baada ya kumuua dada wa kufikia, Anna Thomas (28), kisha kuutumbukiza mwili wake chooni huku akimchoma kisu ubavuni mama yake mzazi.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki katika Mtaa wa Kimamba, Kata ya Makulumla, Ubungo, Dar es Salaam, kwa kijana huyo baada ya kumuua binti huyo. Baada ya kufanya kitendo hicho, alipohojiwa na mama yake, alimchoma kisu ndipo majirani walikasirika, wakamshambulia hadi kufa.

Mwandishi wa gazeti hili jana alishuhudia nyuki wakivamia waombolezaji kwenye makaburi ya Mburahati, Dar es Salaam, na kuwang'ata hali iliyozua taharuki.

Kutokana na hali hiyo, kila mmoja alitawanyika upande wake na kuliacha jeneza halijafukiwa vizuri, huku wakifukuza wadudu hao waliokuwa wamewang'ata baadhi yao.

Tukio hilo lilidumu kwa zaidi ya dakika 15 kila mmoja akiwa ametawanyika akiwamo mchungaji aliyekuwa anaongoza ibada ya maziko.

Hadi Nipashe inaondoka makaburini hapo waombolezaji walikuwa hawajarudi wakisubiri hali kutulia kwa kwua wadudu hao walikuwa wanaongezeka wakizunguka kwenye anga.

Mmoja wa waombolezaji, Anaeli Michael, alisema aliwaona wanafunzi wa shule ya msingi wakiwa mbele wakifuatiwa na mbuzi kwenda eneo la mkusanyiko wa waombolezaji. Aidha, upande wa juu kulikuwa na kundi la kunguru waliotawanyika eneo hilo.

"Kwa kweli hata sijui nyuki hao wanatokea wapi. Tunashangaa tu kuona watoto wanakimbizwa na sisi ikabidi tuache lililotuleta kunusuru nafsi zetu, kama unavyoona nimeng'atwa maeneo ya shingoni na kichwani. Huenda wale wanafunzi waliwachokoza nyuki hao," alisema Anaeli.

Mama wa marehemu huyo, Lonida Mosha, alikubali kushiriki mazishi ya mwanaye baada ya juzi kutoa kauli ya kuwa hatoshiriki kutokana na kitendo cha kinyama alichokifanya ikiwamo kumchoma kisu kwenye mbavu.

Aidha, mwili wa kijana huyo ulizikwa moja kwa moja kutokea Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) baada ya mama huyo, kukataa kuweka msiba nyumbani kwa kuchukizwa na kitendo alichokifanya mwanaye aliyemuua binti wa kufikia aitwaye Anna.

Kijana huyo alimuua binti huyo ambaye mama huyo alimuokota Kituo Kikuu cha Mabasi Ubungo zaidi ya miaka 17 iliyopita.

Nipashe ilitembelea nyumbani kwa Lorinda jana saa 5:00 asubuhi na kukuta hakuna msiba uliowekwa huku Mwenyekiti wa mtaa huo, Ibrahim Mselem, pamoja na majirani wakimbembeleza mama huyo angalau kuhudhuria misa ya kijana wake iliyofanyika katika Kanisa la Baptist, Muhimbili.

"Imebidi tutumie busara kumbembeleza Lorina kushiriki mazishi ya mwanawe kwa sababu alishakataa tangu juzi, alisema yeye atamzika mtoto wake Anna tu, kwa kweli ameumizwa sana kifo cha yule binti, tunashukuru alituelewa na kushiriki,"alisema Ibrahim.

Ulipofika muda wa kutoa salamu za mwisho kanisani mama huyo alijumuika pamoja na familia na marafiki kuuaga mwili wa mwanawe pamoja na kushiriki kuuzika mwili wake makaburini, jambo lililoamsha hisia ya huzuni kwa waliohudhuria msiba huo.

Mchungaji wa Kanisa la Baptist Tanzania, Imani Katana, aliyeongoza misa ya kumuaga marehemu, aliwataka waumini kuacha kuhukumu na kumgeukia Mungu kwa kuwa mbele zake binadamu wote ni sawa.

"Siku ya mwisho roho yako itakwenda kusimama mbele za Mungu na kutoa hesabu ya matendo yako hapa duniani, huko hatutokwenda na miili hii, tutapata miili mipya kwa hiyo ndugu zangu tuyaache matendo ya mwili na tusikize sauti ya Mungu kupitia mioyo yetu,"alisema.

Aidha aliwataka wazazi kufuatilia mienendo ya watoto na vijana wao, wahusike kwa ukaribu katika malezi yao, ili kuwaepusha na matendo ya ukatili yasiyofaa katika jamii, na kuwa Mungu anakaa ndani ya mzazi pale anaposimama katika nafasi yake kwenye malezi.

**KUHUSU BINTI**

Baadhi ya majirani walisema wanashirikiana na mama huyo kupata kibali cha kumzika binti huyo kwa kuwa ndugu zake wako Mwanza. "Baada ya kukaa miaka mitano, mama alimwambia aende akasalimie wazazi wake, alivyofika alikuta wamefariki, bibi yake (Anna) akamtafutia kazi Bukoba mjini, hakupenda akarudi akamwambia wewe ndio mama yangu na nikifa nizikwe huku (Dar),"alisema jirani mmoja.

Siku ya kuzikwa binti huyo haijajulikana kutokana na taratibu za kisheria kwa kuwa ndugu zake wako mbali naye alishasema akifa azikwe Dar es Salaam.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | ITU COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 93457 KIWANJA NAMBA '1', KITALU 'G' MAPINGA ,KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 89175 KIWANJA NA. '1157', KITALU 'A' TEGETA KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA | ANDREW ANTHONY SINDABAHA | 1.MAPINGA BAGAMOYO 2.TEGETA | 22/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 24/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba/Kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0745707008/0759282344**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## PUBLIC NOTICE

### A CALL FOR STAKEHOLDERS' VIEWS ON MULTIYEAR TARIFF APPLICATION SUBMITTED BY ORKESUMET WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY (ORKESUMET WSSA)

On 16th December 2022 the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) received an application for multiyear tariff adjustment from Orkesumet Water Supply and Sanitation Authority (Orkesumet WSSA). Tables 1 to 3 below present tariffs and fees proposed by Orkesumet WSSA.

**Table 1: Current and Proposed Water Tariffs (TZS/m3)**

| Customer Category | Current Tariff | Proposed Tariffs | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Domestic | 2,500 | 2,800 | 3,200 | 3,600 |
| Institutional | 2,500 | 2,800 | 3,200 | 3,600 |
| Commercial | 2,500 | 2,800 | 3,200 | 3,600 |
| Kiosk | 2,500 | 2,800 | 3,200 | 3,600 |

**Table 2: Current and Proposed Reconnection Fees (TZS/Reconnection)**

| Customer Category | Current Fees | Proposed Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| All customers | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

**Table 3: Current and Proposed New Connection Fees (TZS/Connection)**

| Customer Category | Current Fees | Proposed Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Domestic | 20% of recoverable expenditures as stipulated in Section 26 of Water Supply Regulations, 2019 | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Institutional | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Commercial | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Industrial | | 26,000 | 26 ,000 | 26,000 |

According to Orkesumet WSSA, the proposed tariff adjustment will enable the utility to implement activities set out in her business plan for the period from 2022 to 2025 and hence ensure sustainability in provision of portable water and sanitation services to consumers.

Pursuant to Section 19(2) (b) of the EWURA Act, Cap 414, there shall be a public inquiry meeting on **Thursday, 16th February 2023 at Simanjiro Secondary School Hall, Orkesumet Town from 10:00hrs.** The main objective of the meeting is to collect views of stakeholders including Government Consultative Council (GCC), Consumer Consultative Council (CCC), Orkesumet WSSA's customers and the public in general on the reasonableness of the proposed tariff application.

Stakeholders are requested to submit written comments to the Director General though the above-mentioned address at any time by 23rd February 2022. More details of the application can be obtained from **Head Quarters** located at **EWURA House, Medeli West, Dodoma or EWURA Northern Zone Offices,** located at **2nd Floor, PSSSF Plaza, Next to Kibo Palace Hotel, Corridor Area, Arusha** or from **Orkesumet WSSA** offices in Orkesumet town.

**Issued by:**
**Director General**
**EWURA**



Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame (kulia), akionyesha kwa wananchi samaki aina ya sewa, wakati wa uzinduzi wa uuzwaji wa tani elfu 60 za kitoweo hicho, katika soko la samaki la kimataifa la Feri, jijini Dar es Salaam jana, waliovuliwa na meli ya uvuvi ya Pacific Star inayopeperusha bendera ya Tanzania. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Mwigulu akerwa na wabunge kulalamika

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akerwa na michango ya baadhi ya wabunge wanaoeleza tu matatizo bila kutaja suluhisho huku akitaka umakini wa kauli zitolewazo kwa kuwa nchi nyingine huchangia kushusha uchumi.

Aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma wakati akifafanua hoja mbalimbali za wabunge zilizotolewa wakati wakichangia taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

"Ninaomba tuelewane vizuri sana, vinginevyo tutabadilisha Bunge hili kuwa eneo la kujadili matukio. Hiki chombo ni kikubwa sana si cha kujadili tu matukio. Kinatakiwa kishauri serikali namna gani inaweza kuweka mipango yake ya kuwatoa Watanzania kwenye umaskini.

Mwigulu alisema leo kwa sababu inasikika vizuri kwa watu, ukionekana unasemea bei kila mmoja anaiongelea.

"Lakini twendeni kwenye uhalisia, nchi hii ina wazalishaji na walaji, mara zote tukumbuke hili na hivyo vyakula vinavyozalishwa havizalishwi kwa mashamba ya vijiji vya ujamaa, ni watu binafsi wanaingia kuzalisha anajipinda kuzalisha. Wabunge kama watunga sera na sheria lazima wawe makini kuweka uwiano wa hayo maeneo mawili.

"Mtu yupo pale kwenye uzalishaji anasema 'serikali inajificha tu kwenye Ukraine, sisi tumezalisha hapa, kwa nini bei iko juu? Mmezalisha Mwanzugi lakini Mwanzugi hamtengenezi mbolea, mbolea mliyotumia kuzalishia ni ya bei ya juu ndio ile iliyosababisha yale yatakayozalishwa kama mfuko ulitumia wa Sh. 120,000 ni lazima mazao kijijini kwao yatakuwa na bei ya juu," alisema.

Waziri huyo alisema ni lazima wanapoeleza matatizo yaliyopo, waeleze na hatua zilizochukuliwa wasionyeshe ufahari katika kuwatajia Watanzania matatizo kwamba kuna bei wakati wananchi wanazijua na kila siku wananunua vitu.

"Mheshimiwa Mwenyekiti ukiona mara zote kelele zinapigwa kwenye haya mambo ya dharura, kuwa makini sana. Wakati mwingine unaweza kubeba na deal (mambo) ya watu humo humo. Lazima tuwalinde wakulima wetu na lazima tuwalinde walaji wetu," alisisitiza.

Kuhusu hoja ya akiba kushuka kutoka dola bilioni 6,000 hadi dola bilioni 4,500, Mwigulu alisema masomo ya uchumi ni sayansi.

"Twendeni tufuatilie kwa umakini ilipokuwa 6,300 tulikuwa trilioni moja fedha ilikuwa tumeitoa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), sasa tumeichukua ile tumejengea madarasa yote unategemeaje iwe ile ile.

"Haya ndiyo matatizo ya kuonea huruma mbegu, unaogopa kupanda kwa sababu mbegu itapungua, panda ili uvune zaidi. Pia tuna miradi mikubwa kuliko nchi yoyote ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na vitendea kazi tunavyojengea tunaagiza nje, unategemeaje reserve ziwe zile zile tu.

"Hii ni kazi sana kufundisha mtu yule yule ametaka kwa makusudi kutoelewa, haiwezekani tukawa tunatumia muda wa Bunge kujadili kitu kile kile tunataka kupata nini, hatuna mashaka kuhusu 'reserve' (akiba), nchi yetu ipo na zaidi ya miezi minne ya nukta saba importation (agizaji) wastani ni miezi minne tu tuko makini kwenye hilo.

"Hata deni la taifa tuna asilimia 73 ya mikopo yetu tangu uhuru imekopwa kwa concession (makubaliano) ya kipindi cha miaka 10 na kiwango cha riba ni 0.75 ambapo asilimia 26 inayobakia ni commercial (kibiashara) ambayo tumeamua kukopa kwa sababu ni miradi ambayo isingeungwa mkono.

"Tuna uhakika Bwawa la Mwalimu Nyerere litalipa, reli italipa, sasa hapa tunatisha tisha watu nini na kwa ajili ya nini, na sasa niwahakikishe hii si 'Honorable Doctor' (udaktari wa heshima) nimeingia darasani.

"Mheshimiwa Rais Samia mbinu alizochukua na maono aliyoyaleta kwenye masuala ya kichumi si yakutilia mashaka wafuatilieni wabobezi wa IMF, WB (Benki ya Dunia) na wachumi wote wanasema 'uchumi wa Tanzania, uko pazuri na unaelekea pazuri'.

"Haya si maneno ya Mwigulu, IMF wamesema hivyo, WB wamesema hivyo, tuache kujidharau dharau, Watanzania tumezoea sana kujidharau, hata juzi ilielezwa kwamba timu ya Tanzania ni ya tano, jamaa mmoja anasema haiwezekani ligi yetu iwe ya tano," alisema.

## Balozi wa Denmark nchini apongeza utendaji CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Benki ya CRDB ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wake, Abdulmajid Nsekela, umekutana na Balozi wa Denmark nchini, Mette Nørgaard Dissing-Spandet, kujadili uhusiano baina ya Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na benki hiyo.

Majadiliano hayo yamefanyika katika kipindi ambacho benki hiyo kinara wa utoaji huduma za kifedha nchini imetoka kupata faida kubwa kwa mwaka uliopita, ikiivunja rekodi yake yenyewe iliyoiweka kwa mwaka 2021 ya faida baada ya kodi ya takriban Sh. bilioni 268 na kufikia faida ya Sh. bilioni 353 kwa mwaka 2022.

Mafanikio hayo yanaelezwa kutokana na jitihada za makusudi za benki hiyo kukuza vyanzo vya mapato yasiyotokana na riba ambapo yaliongezeka kwa asilimia 13 mwaka hadi mwaka na kufikia kiasi cha Sh. bilioni 400 kutoka Sh. bilioni 354.

Nsekela, akifafanua rekodi hiyo, alisema imechangiwa na ongezeko la ufanyaji miamala ya fedha hususan kupitia njia za kidijitali.

Kiujumla, wanahisa wa benki hii, DANIDA akiwa mmojawapo akishirikiana na Serikali ya Tanzania, wanaendelea kuona fahari ya kuwa sehemu ya uwekezaji wa benki inayofanya vizuri kwa kuwa wana uhakika gawio lao litaongezeka maradufu.

Balozi Dissing-Spandet, akizungumza na viongozi wa Benki ya CRDB, alisema amefurahishwa na matokeo mazuri ya benki hiyo kwa 2022 na ni kiashiria kizuri kwa matokeo yajayo.

**DANIDA na CRDB**

Uhusiano wa DANIDA na Benki ya CRDB haujaanza leo, mizizi yake ilipandwa kupitia uhusiano wa kidiplomasia baina ya Tanzania na Denmark.

Tanzania imekuwa mnufaika wa misaada ya kimaendeleo kutoka kwa Denmark kupitia DANIDA kwa miongo kadhaa iliyopita ikitekeleza miradi ya afya, uchumi, utafiti, ujasiriamali na mingineyo.

Wakati Benki ya CRDB ikijulikana kama Cooperative Rural Development Bank, ilipitia nyakati ngumu kiasi cha kushindwa kujiendesha, hatua iliyopelekea serikali kuiomba DANIDA kupitia Mfuko wa Uwekezaji wa Denmark (DIF) kuinasua benki hiyo.

Kuingia kwa DIF kama mwekezaji kulileta mageuzi katika benki hiyo ambayo 'ilizaliwa upya' kama Benki ya CRDB. Miaka kadhaa baadaye Benki ya CRDB ilifikia hadhi ya kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

DIF ilianza kwa kuwekeza hisa 247,014 mwaka 2002 ambazo zimeongezeka na kufikia hisa 548,067,648 mwaka 2021 ambazo ni sawa na asilimia 21 ya hisa zote za Benki ya CRDB.

Katika upande wa gawio, DIF na Serikali ya Tanzania, zilipata kiasi cha Sh. milioni 247 mwaka 2002 na Sh. bilioni 19.7 mwaka 2021.

Nsekela alisema uhusiano huo wa aina yake baina ya DANIDA, serikali na Benki ya CRDB umekuwa na maana kubwa katika kuifanya benki hiyo kuendelea kufanya vyema kila mwaka na kupata faida katika biashara yake.

Serikali ya Denmark imeendeleza ushirikiano wake na Benki ya CRDB na sasa imewekeza kupitia mfuko wake wa Uwekezaji unaoitwa Investment Fund for Developing Countries (IFU), kwenye Kampuni tanzu ya Benki ya CRDB Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kwa kuwa DANIDA ni mdau wa maendeleo nchini, inaelezwa kuwa Denmark ilikuwa miongoni mwa waasisi wa Fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF) mwaka 1999 na imekuwa ikiendelea kuchangia katika mfuko huo. Kwa mwaka huo pekee, ilichangia kiasi cha DKK milioni 60.

Kupitia mchango wake katika fedha za mifuko ya afya ya pamoja kwa bara na visiwani, DANIDA imekuwa ikitumia fedha zake za uwekezaji kusaidia kuboresha mifumo ya afya, ubora wa huduma za afya, huduma za afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana.

HABARI KITAIFA



Ofisa Mwandamizi wa Jinsia, Wanawake, Watoto na Watu wenye Ulemavu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ambaye ni Mratibu wa Mtandao wa Kupinga Ukeketaji Tanzania, Getrude Dyabena, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati akitoa mapendekezo nane ya mtandao huo kuhusu kusaidia kutokomeza vitendo vya ukeketaji nchini. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mnyeti kortini kwa madai matumizi mabaya madaraka

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MBUNGE wa Misugwi na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amefikishwa mahakamani kwa madai ya matumizi mabaya ya madaraka.

Mnyeti alifikishwa jana katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha mbele ya Jaji Mfawidhi John Kahozya na Kampuni ya Uwindaji ya HSK Safaris ya Simanjiro mkoani Manyara kwa madai ya kuisababishia hasara.

Licha ya kushtakiwa mahakamani, Mnyeti hakufika badala yake aliwakilishwa na wakili wake, Kuwengwa Ndojekwa, ambaye aliiomba mahakama imruhusu aiunganishe serikali kwenye kesi kwa sababu yale anayodaiwa kuyatenda yalifanyika akiwa mkuu wa mkoa wa Manyara na alikuwa mtumishi wa umma.

Mnyeti, ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo, anadaiwa kushirikiana na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Emboreet, Salehe Alamry, ambaye ni mshtakiwa namba mbili kuinyang'anya kampuni hiyo kitalu cha uwindaji bila kufuata sheria. Mdaiwa wa tatu katika kesi hiyo ni Salehe Alamry.

Wakati Mnyeti anawakilishwa na Wakili Ndejekwa, Salehe Alamry, anawakilishwa na Wakili Sheki Mfinanga na HSK Safaris Ltd inawakilishwa na Edmond Ngemela.

Ilielezwa mahakamani hapo na jaji kuwa wakili wa Alamry alitakiwa kuchukua nyaraka na hatua stahiki za kuitwa shaurini ila badala yake alikuja na blabla.

Vile vile mahakama ilibaini Salehe Alamry alipokea hati ya kuitwa shaurini ila kwa kiburi alikataa kuzipokea.

Jaji Kahyoza alisema pamoja na kuwaruhusu wajibu madai ndani ya siku 10, ameona kuna sababu za ucheleweshaji zisizo na msingi.

# Lissu asimulia maisha yake Ubelgiji

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesimulia ugumu wa maisha aliyoyapitia kipindi chote alichokuwa akiishi uhamishoni nchini Ubelgiji.

Aliweka wazi hayo katika mahojiano maalum na kituo cha runinga cha ITV kupitia kipindi chake cha 'Dakika 45' kilichorushwa usiku wa kuamkia jana.

"Ukilazimika kuondoka nyumbani kwako au kwenu na kwenda kuishi mahali pengine kwa lazima kwa sababu ya hofu ya maisha yako ni maisha magumu. Nimekaa nje ya Tanzania zaidi ya miaka mitano. Maisha ya ughaibuni ni ya shida sana. Siyo ya bata hasa kama unaishi uhamishoni kwa namna nilikuwa naishi mimi.

"Watu wanafikiria Ulaya fedha zinaokotwa barabarani sijui kama kitu gani, siyo. Vitu ni vizuri ndiyo lakini vinahitaji fedha, kwa hiyo siyo maisha ya bata," alisema.

Lissu alisema kwa sasa amerejea nyumbani moja kwa moja isipokuwa kama atalazimika kusafiri kwenda nje ya nchi ni kwa ajili ya matibabu au shughuli za kikazi na kisiasa.

"Kwa hali yangu ilivyo, nahitaji kuangalia afya mara kwa mara, itabidi niwe natoka. Lakini kwa kazi yangu ya siasa pia, nina shughuli nyingi za kimataifa ambazo zinahitaji nitoke. Kwa hiyo habari kutoka nje itakuwapo kama ambavyo ilikuwapo kabla sijaenda uhamishoni,"alisema.

**AKATAA 'UCHAWA'**

Lissu alisema hataki watu wanaojiita chawa na hayuko tayari kuwa na chawa wake wala yeye kuwa chawa wa mtu.

"Labda kwa sababu nimekaa nje muda mrefu. Yamenipita mengi, lakini watu kukubali kuitwa chawa, mdudu anayepatikana au anayetokana na uchafu. Watu wakubali kuitwa chawa na wanachekelea, hiyo ni shida sana.

"Kwa hiyo kama kuna mtu anafikiria kuwa chawa wangu, haina budi nimwambie anipishe kwanza. Sitaki kuhusishwa na chawa, chawa ni uchafu. Sitaki kuwa chawa wa mtu yeyote, sitaki mtu yeyote awe chawa wangu. Nataka raia wanaojitambua," alisisitiza.

**UENYEKITI CHADEMA**

Akizungumzia madai kwamba anataka uenyekiti wa chama hicho, Lissu alisema hajawahi kutaka nafasi hiyo.

"Kuna mtu aliniuliza kwamba nataka uenyekiti, nikamwambia sijawahi kuota kuwa mwenyekiti wa chama. Kwa hiyo haya maneno maneno wanajaribu kutuchonganisha, wameshindwa kutuangamiza, kutuondolea maisha, wameshindwa kutufunga, sasa wanafikiria watatugawa," alisema.

**MBOWE KULAMBISHWA ASALI**

Kuhusu madai ya Mbowe kulambishwa asali, kwa maana ya kuwa kibaraka wa serikali, Lissu alisema tuhuma hizo ni vitu vinavyotengenezwa kuwachafua.

"Mwenyekiti wetu (Mbowe) ameumizwa sana. Alikuwa na biashara nyingi, zimevurugwa zote. Ameingizwa kwenye hasara ya mabilioni mengi sana na endapo angelipwa fedha kutokana na uharibifu aliofanyiwa, ingekuwa sahihi kabisa lakini hajawahi kulipwa madai yake mpaka leo. Halafu anaenda Ikulu anaambiwa amelambishwa asali!" alishangaa.

Kuhusu yeye kuitwa kibaraka, alisema wanaosema hivyo ni wale ambao hawajawahi kupata misukosuko ya kisiasa.

"Kwa watu ambao hawajawahi kutendewa tuliyotendewa sisi kufungwa, kushambuliwa na kuumizwa, wanachama au viongozi wao hawajawahi kuuawa, kuteswa kwenye vituo vya magereza na polisi. Hawawezi kujua adha ambayo tumeipitia sisi ambao tumepitishwa kwenye hilo tanuli la moto.

"Nimepigwa risasi 16. Nilivyokuwa nakuja miaka mingi iliyopita ITV, sikuwa kilema. Leo natembea wananiita 'Chiba' ambaye miguu yake ni imara. Nimekuwa hivyo kwa sababu nimepigwa risasi. Sasa nikiambiwa kwamba kuna watu wanataka kuja kukudhuru, natakiwa kuchekelea au nichukue hatua? alihoji Lissu.

"Katika mazingira yaliyonifanya nikapigwa risasi na mtu anapozungumza vibaraka, inabidi tumuulize huyu anaishi Tanzania ipi ambaye hawezi kuona yale ambayo tumefanyiwa sisi (CHADEMA)," alisema.


**LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)**
**PUBLICATION OF BI-ANNUAL INCOME AND EXPENDITURE.**

Lawyers' Environmental Action Team is a Non-Governmental Organization which was founded in 1994 and is registered under the NGOs Act of 2002 with (Certificate of Compliance No. 1985).

**Vision:** Tanzania with sustainable and well-managed environment and natural resources for current and future generations.

**Mission:** To contribute towards good governance in the use and sustainable management of the environment and natural resources through public interest litigation, advocacy, strategic research, capacity building, and networking.

In accordance with Non-Governmental Organization (Amendment) Regulation, 2018, Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) is pleased to publish the amount of funds received and expended from July, 2022 to December, 2022.

**Bi-Annual Income and Expenditure for the period from July 2022 to December 2022**

| **Income:** | **TZS** |
|---|---|
| Receipt from Donors | 932,987,905.82 |
| **Total Income** | 932,987,905.82 |
| **Expenditure on:** | |
| Examining the Extractive Industry Legal Regime in Tanzania | 143,922,809.81 |
| Usimamizi Endelevu wa Maliasili in Tanzania | 723,176,774.02 |
| Collective Action for Rights Realization in the Extractive Industry | 61,496,113.99 |
| Human & Admin Resources Activities | 4,392,208.00 |
| **Total Expenditure** | **932,987,905.82** |

In sum, LEAT received grants from the following donors: Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), United States Agency for International Development (USAID-Tanzania); and VSO-Tanzania.

**Lawyers' Environmental Action Team (LEAT),**
**Mazingira House, Mazingira Street,**
**Mikocheni B, House No 8,**
**P.O. Box 12605, Dar es Salaam.**
**Email: info @leat.or.tz.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Busara, hekima vitawale kumpata mkuu Anglikana

**KANISA** la Anglicana Tanzania, wiki hii linatarajia kufanya uchaguzi wa Askofu Mkuu, atakayeliongoza kwa miaka mitano ijayo. Uchaguzi huo unafanyika baada ya kiongozi wa sasa, Dk. Maimbo Mndolwa, kumaliza kipindi chake cha miaka mitano.

Kwa mujibu wa katiba ya kanisa hilo, kila baada ya miaka mitano, unatakiwa kufanyika uchaguzi wa Askofu Mkuu. Iwapo Askofu Mkuu aliyeko madarakani ametumika kipindi kimoja, anaweza kupendekezwa na kuchaguliwa kuongoza kanisa hilo kwa kipindi kingine cha miaka mitano na baada ya hapo anakoma kuwa kiongozi mkuu wa kanisa hilo ambalo ni la tatu kwa ukubwa nchini.

Pamoja na kuwapo kwa utaratibu huo, kwa miaka ya karibuni, viongozi wanaochaguliwa kuongoza kanisa hilo, wamekuwa wakidumu kwa kipindi kimoja na kuondolewa au kuamua kung'atuka. Maaskofu Dk. Valentino Mokiwa na Dk. Jacob Chimeledya walikaa kipindi kimoja kila mmoja. Hatua hiyo ilionyesha kuwa kuna mambo ambayo hayaendi sawa ndani ya taasisi hiyo nyeti. Hiyo ni tofauti na Askofu Dk. Donald Mtetemela na Askofu John Ramadhani ambao walikaa katika nafasi hiyo kwa miaka 14 na miaka 10, mtawalia.

Huku wajumbe wa mkutano mkuu wa kanisa, yaani Sinodi, wakijiandaa kutimiza wajibu huo, kumekuwa na taarifa zinazosambazwa kwamba hali si shwari ndani ya nyumba ya maaskofu na kuna mpango wa kuwapo mabadiliko ya nafasi hiyo. Kwa maneno mengine, wajumbe wamedhamiria kupata Askofu Mkuu mpya, hivyo kuendeleza historia iliyowekwa miaka 10 iliyopita.

Ili kutimiza azma hiyo, kumekuwa na taarifa za makundi yanayochafuana liliwamo lile la kumpaka matope kiongozi aliyemaliza awamu ya kwanza na ana uwezekano wa kugombea tena. Yote hiyo ni kujaribu kumchafua ili asiendelee na uongozi katika ngazi ya juu ya kanisa kwa maslahi ya kundi au makundi ya watu wasioitakia mema taasisi hiyo.

Ni dhahiri kwamba ndani ya kanisa, hususan katika nyumba ya maaskofu, kuna mpasuko mkubwa ndiyo maana kunakuwapo na taarifa za makundi yanayochafuana na kupakana tope miongoni mwao. Jambo hilo pamoja na kashfa mbalimbali za kurushiana miongoni mwa maaskofu huku wakituhumiana kwa ubadhirifu na ukosefu wa maadili, linaliweka kanisa katika hali ya hatari na kuondoka kabisa kwenye misingi na malengo ya kuanzishwa kwake.

Kanisa la Angilkana, ukiacha Kanisa la Katolini na lile la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) moja ya makanisa yenye waumini wengi na mfumo wenye kueleweka katika uongozi na mfumo wa uendeshaji.

Kuwapo kwa tuhuma za kuchafuana miongoni mwa viongozi kisa ni nafasi ya Askofu Mkuu, ni dalili kwamba kuna mwelekeo wa kupoteza dira, kutoweka kwa amani na mshikamano huku ubinafsi na maslahi binafsi au ya vikundi vya watu vikitamalaki.

Ni dhahiri kwamba kuna wazee waliowahi kushika nafasi za uongozi ndani ya kanisa hilo kama vile Askofu Dk. Mtetemela, Askofu Dk. Simon Kiwanga, Askofu Dk. Chimeledya, Askofu Dk. Valentino Mokiwa, Askofu Dk. Maternus Kapinga na wengine. Wazee hao pamoja na wale wenye busara wanaotoka katika kanisa hilo, akiwamo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi Maalum) wanapaswa kutumika kuepusha mpasuko zaidi ndani ya kanisa hilo.

Tunasema hivyo kwa sababu baadhi ya wazee hao na walei wenye hekima, ni watu wa muhimu katika kutazama na hatimaye kuonya baadhi ya mambo yasiyofaa yanayoendelea ndani ya taasisi hiyo iliyojijengea heshima ili kurejesha umoja na mshikamano ndani ya nyumba ya maaskofu.

Ni vyema busara ikatumika zaidi katika Mkutano Mkuu wa Sinodi ya Kanisa ili kuwawezesha wajumbe kutumia busara na hekima katika kupata kiongozi atakayeliongoza kanisa badala ya mtu astakayechaguliwa kwa shinikizo la watu wachache na hatimaye kuzidi kuligawa kanisa na kuharibu kusudi la Mwenyezi Mungu kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Happy birthday' CCM, ijapange

Na Sabato Kasika

**CCM** miongoni mwa vyama vikongwe vya siasa barani Afrika vilivyoko madarakani, Jumapili iliyopita imetimiza miaka 46, 'happy birthday CCM'.

Februari 5, 1977 ilizaliwa CCM baada ya kuunganishwa TANU na Afro Shiraz ya Zanzibar, ni pongezi nyingi kwa chama miaka 46 si haba, kutokana na ukweli kwamba, vyama vingi vikongwe barani Afrika vilishawekwa pembeni.

CCM inakubalika na imeendelea kuwaongoza Watanzania na kusimamia maendeleo kuanzia uchumi, demokrasia, mtangamo wa kisiasa, maridhiano na siasa za uhimilivu.

Vyama vikongwe vimeanguka baada ya wimbi la mageuzi ya mfumo wa vyama vya vingi lilipotua Afrika mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Hata hivyo, wakati CCM inatimiza miaka 46, chama hicho hakina budi kujitafakari na kujituma badala ya kubweteka, kwa kuweka mikakati ambayo itakifanya kuendelea kushika dola.

Ninashauri hivyo, kwa sababu kumekuwapo na tuhuma za muda mrefu kutoka ndani ya chama kuhusu baadhi ya makada kukengeuka kwa kujihusisha na rushwa, ambayo ni adui wa haki, hivyo kama mwanachama anadhulumiwa haki yake, anaweza kuchukua maamuzi magumu ikiwamo kuhama au kuachana na siasa.

Hivyo, wakati huu ambao chama kimetimiza miaka 46, ni vyema pia wanachama kurejea katika ahadi 10 za mwanachama ambazo zimejipambanua wazi jinsi kada anavyotakiwa kuwa.

Mfano ahadi ya nne inasema; rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa", lakini pamoja na kuwapo kwa ahadi hiyo rushwa inalalamikiwa.

Katika uchaguzi unaofanyika ndani ya chama, wapo ambao hulalamika wakidai kuenguliwa katika mchakato wa kura za maoni au kunyimwa fomu za kuwania uongozi.

Hata katika uchaguzi wa mwaka jana, matukio hayo yalijitokeza hadi uongozi wa juu wa chama uchaguzi kurudiwa upya mchakato chanzo kikuu kikihusishwa na mlungula.

Viongozi wakuu wa chama wanakemea hivyo wakati wa maadhimisho wakati huu chama kimehitimisha miaka 46 ya kuzaliwa kwake, kiweke mikakati imara ya kukomesha rushwa hiyo.

Hilo likifanyika, litaendelea kuwajengea imani wanachama na wapenzi wa CCM na kuwafanya waendelee kukitetea wakati wote.

Lakini Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, alielekeza wanachama wakubali kukosolewa, wajibu mashambulizi ya wapinzani kwa hoja.

Kilichosemwa na Mwenyekiti wa CCM ni sahihi, hasa kutokana na ukweli kwamba ni chama kikongwe, hivyo wanachama wake ni vyema waonyeshe ukomavu katika siasa.

Hivyo, maadhimisho ya miaka 46 ya kuzaliwa CCM, iwe ni fursa kukaa na kutafakari na kuondokana makandokando yote ili iwe rahisi kutumia mikutano ya hadhara kujibu hoja za upinzani bila hofu.

Ninaamini kwamba, chama kikijipanga na kuepuka kasoro zikiwamo za rushwa, ni rahisi kusimama na kujibu hoja za upinzani kwa kujiamini, hasa kutokana na ukweli kwamba vyama hivyo vina hoja mbalimbali ambazo ni muhimu zijibiwe kwa hoja siyo porojo au kupayuka.

Bila kujipanga kikamilifu, vyama hivyo vinaweza kuitoa CCM kwenye reli kwa hoja nzito. Ndiyo maana nikashauri kuwa ni muhimu kujipanga, hasa kwa kujisafisha kwanza dhidi ya tuhuma mbalimbali zikiwamo za rushwa.

Kama anavyoagiza Mwenyekiti kuwa CCM inapokosolewa ichukue hoja za upinzani na kuzifanyia kazi, hili ni jambo jema, kwani upinzani ukitumika vizuri unaweza kuwa ni kioo cha kuangalia kasoro na kuzirekebisha.

Kazi ya kioo ni kumwonyesha mtu kasoro katika mwili wake na kujirekebisha, iwapo kioo kitamwonyesha mtu kasoro halafu akakivunja, ataendelea kuchafuka bila kujua.

Jambo lingine la kutambua ni kwamba, kufanya siasa kwa mazoea kumeshapitwa na wakati, hivyo ni muhimu makada kutetea chama kwa kujenga hoja nzito zinazoonyesha ukomavu wa kisiasa.

## Upelelezi kesi anayedaiwa kumuua mke kwa magunia mkaa ngoma nzito

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashtaka katika kesi ya tuhuma za mauaji inayomkabili mfanyabiashara Khamis Luwonga (38) anayeshtakiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani, kwa kumchoma moto kwa kutumia magunia ya mkaa, umeieleza mahakama kuwa bado kuna majalada matano yanafanyiwa marekebisho ili yapelekwe Mahakama Kuu.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Mosie Kaima, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalila wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Alidai kuwa kesi iliitwa kwa ajili ya kutajwa na bado kuna majalada matano hayajakamilika kuna marekebisho yalipelekwa polisi kwa ajili ya kurekebisha ili yapelekwe Mahakama Kuu.

"Bado kuna vijalada vitano kwenda Mahakama Kuu havijakamilika kuna marekebisho yalipelekwa polisi kwa ajili ya kurekebisha vijalada hivyo," alidai Kaima.

Hata hivyo, jopo la mawakili watatu wa mshtakiwa, Zidadi Mikidadi, Mohamed Majaliwa na Fatuma Abdul, lilidai kuwa ni mara ya tano kesi hiyo inaahirishwa kwa madai kuwa upelelezi haujakamilika, hivyo upande wa mashtaka umekiuka Sheria ya Mwenendo wa Jinai.

Kutokana na hali hiyo, Mikidadi alidai kuwa wamefungua maombi Mahakama Kuu ili wapate maelezo ya uhalali wa kesi namba 5/2022 ya mauaji baada ya kesi ya awali ya mshtakiwa huyo kufutwa na kufunguliwa upya. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Februari 20, mwaka huu, itakapotajwa.

Awali, mshtakiwa Luwonga alimwomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuishughulikia ofisi ya waendesha mashtaka kwa kushindwa kumjibu barua zake alizokiri kuwa alimuua mkewe bila kukusudia.

Pia alidai kuwa wakati yuko kituo cha polisi na kwa mlinzi wa amani, alikiri pia kumuua mkewe huyo bila kukusudia kwa kuwaeleza ukweli wote tukio hilo lilivyotokea hadi mkewe kupoteza maisha.

"Nakuomba Mheshimiwa Hakimu unipe dakika mbili nizungumze kidogo. Kuna jambo linanishangaza sana na ni la ajabu kuna baadhi ya wafanyakazi wa upande wa mashtaka wanafanya mambo ya ajabu sana.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan naomba ushughulikie watumishi hawa kwa sababu nimeshaandika barua ya kukiri kumuua mke wangu Naomi bila kukusudia lakini hadi leo (jana) wananizungusha wana kazi ya kuondoa kesi na kuileta mpya," alidai Luwonga.

Pia alidai ofisi hiyo si nzuri hata kidogo kwa sababu hata kipindi cha marehemu Rais Dk. John Magufuli, aliandaa barua katika ofisi ya waendesha mashtaka lakini hajajibiwa.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba 4/2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kuwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

Anadaiwa kumuua mke wake kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na alichukua majivu kwenda kuyafukia shambani kwake.



Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero (KSCL), Ephraim Mafuru, akizungumza na waandishi wa habari katika Bandari ya Dar es Salaam mapema wiki hii, baada ya kuwasili kwa vifaa vya mradi wa upanuzi wa kiwanda cha KSCL, unaoendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024, ikiwa ni juhudi za kampuni hiyo kuunga mkono lengo la serikali la kufikia kujitosheleza kwa sukari nchini. Kushoto ni Meneja Mwandamizi wa TSK Tanzania, Mei Shirin Bomassy. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Daktari atoa somo kuhusu kifafa

**Na Christina Mwakangale**

JAMII imeshauriwa kutohusisha ugonjwa wa kifafa na sababu zilizo nje ya kisayansi, ikiwamo dhana kwamba ni maradhi ya kulogwa na yasiyotibika.

Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Fahamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Tawi la Mloganzila, Dk. Brighton Mushengezi, alisema hayo jana, Dar es Salaam kwenye mahojiano maalumu na Nipashe kuelekea Siku ya Kifafa Duniani.

Alisema uelewa kuhusu ugonjwa huo nchini bado ni mdogo kwa jamii, hivyo siku hiyo hutumika kuelimisha umma ili kufahamu dalili, sababu na athari za ugonjwa huo ambao hauchagui umri.

"Kuna tafsiri na dhana tofauti kwa jamii kwamba mtu akiumwa kifafa amelogwa, hivyo kuwafanya watu kwenda kutibiwa na dawa za kienyeji, wengine wanatumia dawa za hospitalini na za kienyeji pia huku mwingine akienda kwenye nyumba za ibada tu bila tiba," alisema.

"Wako wanaochanganya degedege na kifafa jambo ambalo halina uhusiano. Degedege ni tukio la kupoteza fahamu linalosababishwa na sababu kadhaa ila kifafa ni ugonjwa ambao mtu hupoteza fahamu au asipoteze fahamu," alisema Dk. Mushengezi.

Alisema ugonjwa huo huweza kumkumba yeyote na mahali popote ikiwamo kazini huku akibainisha kuwa chanzo ni mfumo wa umeme kwenye ubongo kuhitilafiwa kwa sababu ya ajali, uvimbe au wakati mtoto anapozaliwa.

"Kwenye ubongo pakishaweka kovu, kama ni sehemu ya umeme ambako hapahitaji kusumbuliwa ndiyo matokeo ya kifafa. Utakuta mwingine anakuja hapa ni dereva anasema udereva ndiyo maisha yake, hivyo apewe dawa aendelee na shughuli zake, ila kuna hatari," alisema.

Dk. Mushengezi alisema duniani, wanaougua kifafa wamefikia milioni 67 akisema wanaotumia tiba ya dawa kwa usahihi kwa asilimia 70 kutokana na muda waliopangiwa, hupona kabisa.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Mbunge ahoji uhalali wa malipo ya kujifungua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Temeke (CCM), Dorothy Kilave ameitaka serikali kupunguza gharama za malipo kwa kinamama wanaojifungua kwa njia ya kawaida na wale wanaohitaji upasuaji.

Akiuliza maswali bungeni jijini hapa jana, mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kupunguza gharama za mjamzito anapojifungua kwa upasuaji, akibainisha kuwa Hospitali ya Wilaya ya Temeke wanalipa Sh. 200,000 huku kwenye vituo vya afya wanalipa Sh. 100,000.

"Kuna mkakati gani wa kufanya sasa serikali itoe vifaa ili wanawake wanaokwenda kujifungua wasinunue pamba na viwembe?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alisema Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inayoelekeza kutoa huduma za matibabu bila malipo kwa makundi maalum, wakiwamo wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Alisema kwa vituo vya binafsi visivyo na ubia na serikali, Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote utakapopitishwa utakuwa suluhisho la tatizo hilo.

Alisema mjamzito na mtoto chini ya miaka mitano hawatakiwi kulipishwa na kuwataka wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia takwa hilo la kisera.

"Nimetembea Dar es Salaam nilichogundua ni kwamba unakuta kituo cha afya kina wagonjwa wengi kuliko baadhi ya hospitali za wilaya, kwa mwaka watoto zaidi ya 160,000 wanazaliwa, mgawo wanaopata MSD (Bohari ya Dawa) ni mdogo kulingana na idadi ya watu, tutaliangalia hili," alisema.

Aliongeza kuwa MSD imenunuliwa vifaa vya kutosha kwa ajili ya kinamama wanaojifungua.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Agnes Hokororo alihoji sababu za kutoza fedha huduma za afya kwa watoto njiti ilhali Sera ya Afya inaelekeza huduma hizo zitolewe bure kwa watoto chini ya miaka mitano.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema utoaji wa huduma za afya kwa watoto chini ya miaka tano, wakiwamo njiti kwa vituo vya serikali na vile vya binafsi vilivyo na ubia na serikali ni bure na ni matakwa ya Sera ya Afya.

"Ukamilishaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote utamaliza utata huu kwa wananchi wanaotibiwa kwenye vituo binafsi vya huduma za afya," alisisitiza.



Balozi wa Denmark nchini, Mette Nørgaard Dissing-Spandet (wa pili kulia), akiwa pamoja Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (kulia), Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Neema Mori (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, wakati walipomtembelea ofisini kwake, jijini Dar es Salaam jana, kujadili uwekezaji wa DANIDA ndani ya benki hiyo na mkakati mpya wa miaka mitano wa biashara wa Benki ya CRDB wa 2023/2028. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Programu yazinduliwa kuinua wahitimu wa kike

**Na Mwandishi Wetu**

PROGRAMU ijulikanayo STEM imezinduliwa ili kuwakwamua wahitimu wa kike kwa kutoa mafunzo ya vitendo, ujuzi na fursa za kukuza taaluma.

Lengo la programu hiyo pia ni kuziba pengo la kijinsia katika sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi visiwani Zanzibar kupitia Mradi wa Maendeleo ya Majengo Yanayouzwa kwa Kasi Zaidi (CPS).

Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa CPS, Katrin Dietzold, alisema madhumuni ya programu hiyo ni kutoa jukwaa la kukuza na kuwawezesha wahitimu wa kike kufikia uwakilishi wa juu katika sekta ya uhandisi.

Mpango huo ulianzishwa na Mary Kimonge ambaye ni Mpima Ardhi wa CPS kupitia mpango wa usaidizi wa vipaji ujulikanao kama Leapers wa CPS.

Akikaribisha kundi la kwanza la wahitimu wanne waliohitimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), Dietzold alisema mji wa Fumba, Zanzibar unatoa fursa za kipekee za kujifunza kwa vitendo kwa wahitimu wa kike wa fani hizo.

Wahitimu wanne waliohitimu mafunzo hayo ni mwanafunzi wa usanifu, Sultana Mohammed Nassor (24), sayansi ya mazingira, Emelda Mkarios Mashell (25) na wahitimu wa uhandisi Doreen Damian Saru, Debora Erick Baruta, wote wakiwa na umri wa miaka 24.

"Kuna kazi nyingi za maendeleo na ujenzi katika mji wa Fumba, kwa hiyo wanafunzi wetu watapata fursa ya kutosha ya kupokea ustadi wa hali ya juu na wa vitendo katika fani zao walizochagua.

Mratibu na Mwanzilishi wa Mpango huo, Kimonge, alisema CPS inaamini katika kuwezesha na kuendeleza jamii kwa kutoa jukwaa la ujuzi na maendeleo ya kazi kwa vijana.

"Mradi wa Fumba Town pia umekuwa msaada mkubwa kwa maendeleo ya uchumi wa nchi na unaingiza zaidi ya dola milioni 60 katika uchumi na kutoa mikataba ya ujenzi na huduma kwa kampuni za ndani ambazo hutoa ajira kwa mamia ya wakazi wa eneo hilo wanaoishi karibu na mradi," alisema.

# 'Vijana changamkieni fursa kilimo, ufugaji'

**Na Restuta James**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ametaja fursa zilizoko kwenye sekta hizo huku akiwataka vijana na Watanzania kuzichangamkia ili kukuza kipato cha familia na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Waziri Ndaki, alitaja fursa hizo kuwa ni ufugaji na uvuvi wa kibiashara badala ya ule wa kujikimu unaofanyika sasa.

Alisema wizara inatekeleza mpango wa Samia Ufugaji kwa Tija (SAUTI), unaolenga kuwapa vijana mbinu bora za ufugaji, ili kujiajiri na kuzalisha ajira kwa wengine.

"Hii programu mwasisi wake ni Rais (Samia) mwenyewe. Alitupa maelekezo na sisi tumeshaanza kuitekeleza na tayari tuna vijana 240 wako kwenye vituo atamizi vinane wanajifunza ufugaji kwa vitendo," alisema.

"Kila mmoja tumempa ng'ombe 10, afuge kwa miezi mitatu awauze, akanunue wengine awafuge na kuwauza tena ndani ya kipindi hicho," aliongeza.

Waziri Ndaki alisema mbali na mafunzo hayo ya vitendo, vijana hao wameunganishwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), na kwamba baada ya mwaka mmoja, wafungue biashara ya ufugaji wa kibiashara.

"Pia anapoondoka hapa kwetu ataondoka na hela alizokuwa akiuza wale ng'ombe 10 kila baada ya miezi mitatu kwa hiyo ataondoka na mtaji," alisema.

Ndaki alisema mwaka ujao wa fedha wa 2023/24 chini ya SAUTI, wizara inakusudia kutoa mafunzo kwa vijana wengi zaidi na kwamba ni utekelezaji wa mpango wa mabadiliko wa miaka mitano wa sekta hiyo ambao ulianza mwaka wa fedha 2021/2022.

Kuhusu maziwa, Waziri Ndaki alisema serikali imeanza kujenga vituo vya kukusanya maziwa nchi nzima na kwamba kwa mwaka huu wa fedha, zaidi ya vituo 20 vimejengwa.

Alisema vituo hivyo vimejengwa katika baadhi ya wilaya za mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Njombe na Iringa) Mashariki (Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro na Arusha) na maeneo machache ya Kanda ya Ziwa; ambako kuna wafugaji wanaofuga kibiashara.

"Nitoe wito kwa vijana, maziwa ni biashara na hii ni fursa kwa sababu ni wachache sana walioko kwenye kuchukua maziwa kutoka kwa wafugaji kuyapeleka sokoni au kwenye vituo," alisema.

Katika sekta ya uvuvi, Waziri Ndaki alisema serikali ina miradi ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba na nchi kavu kwa kujenga mabwawa.

"Sasa hivi tuna vijana 200 ambao tumewaweka kwenye vituo 14 vya binafsi na viwili vya kwetu vya serikali. Tunataka kuanza ujenzi wa vizimba na tunategemea wanufaika 1,800 ambao wengi ni vijana," alisema.



# Waliovunjiwa nyumba wamwomba Rais Samia kuwasaidia kulipwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI 43 waliokuwa na nyumba za makazi na biashara pembezoni mwa Barabara ya Mianzini -Timbolo, wamemwangukia Rais Samia Suluhu Hassan, kumwomba awasaidie walipwe fidia wanazodai baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Arusha kuwapatia cheti cha malipo.

Wananchi hao wanaomba kulipwa fidia ya zaidi ya Sh. bilioni 1.740 kutoka na madai ya kwamba Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru ilivunja nyumba hizo ili kupanuliwa na kujengwa kwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Akizungumza jana na Nipashe, Fanuel Silamai, ambaye ni mwenyekiti wa waathirika waliovunjiwa nyumba hizo, alisema endapo hawatalipwa fedha zao watarudi mahakamani kuweka zuio la kusimamisha ujenzi kuendelea kwa kuwa agizo la Mahakama litakuwa limekiukwa.

"Mahakama imetupatia cheti cha malipo ya fedha tunazodai na ilitoa amri kuwa barabara isiendelee kutengenezwa mpaka watakapotulipa, hivyo endapo hawatatulipa tutakwenda mahakamani kuweka zuio la ujenzi kuendelea hadi hapo watakapotekeleza agizo la Mahakama,"alisema.

Alisema madai hayo yamechukua muda mrefu bila kulipwa na kusababisha baadhi kupoteza maisha huku wengine wakiwa ni wagonjwa.

"Madai yetu yamechukua muda mrefu hadi kusababisha watu wanne kupoteza maisha bila ya kulipwa huku wengine wakiwa wamelala kitandani kwa kuwa ni wagonjwa.

"Tunamwomba Rais Samia atusaidie hizi fedha zilipwe kwa kuwa wako waliochukua mikopo benki wameshindwa kulipa na wapo katika hali mbaya kwa kuwa nyumba hizo, zilikuwa za makazi na biashara, pia kuna watu hadi sasa hawana sehemu za kuishi hivyo wamekimbilia kwa ndugu, jamaa na marafiki," aliongeza.

Aidha, alisema mwaka 2011 walipewa taarifa na halmashauri hiyo kuvunja nyumba hizo kwa kuwa barabara ilitakiwa kupanuliwa na waliona hawajetendewa haki, hivyo walikwenda mahakamani na Mei 26, mwaka 2014 walishinda kesi na ilitakiwa walipwe fidia kabla ya ujenzi kuendelea.



Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Laick Gugu (wa pili kushoto), akiwaongoza viongozi mbalimbali wa chama hicho, wakati walipotembelea Kituo cha Afya cha Mkuzi, wilayani humo juzi, katika maadhimisho ya miaka 46 kuzaliwa kwa chama hicho juzi. Viongozi hao na wanachama pia walifanya usafi wa mazingira na kutoa zawadi kwa wagonjwa waliolazwa kituoni hapo. Kulia ni Katibu wa CCM wa wilaya hiyo, Simon Leng'ese. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# RC aomba uhamasishaji zaidi chanjo saratani shingo ya uzazi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, amewataka viongozi wa dini, wanasiasa na wataalamu wa masuala ya afya mkoani humo, kuhamasisha wananchi kutambua umuhimu wa chanjo ya kuzuia saratani ya shingo ya uzazi kwa wasichana wenye umri wa miaka 14.

Alisema kuna umuhimu kwa wadau hao kuhamasisha watu juu ya chanjo hiyo na nyingine za kawaida, zinazotolewa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, ili kupunguza magonjwa yanayoweza kusababishwa na kutokupewa chanjo hizo.

Akizungumza jana kwa niaba ya Mongela, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Ramadhani Madeleka, alisema mbali na chanjo hiyo, wadau wanawajibu wa kuhamasisha jamii kuongeza nguvu kwenye matumizi ya chanjo.

Alisema hayo katika kikao maalum cha kutambulisha mradi wa chanjo, unaotekelezwa na Taasisi za Girl Effect na Gavi the Vaccine Alliance, kwa kushirikiana na serikali kilichoshirikisha wajumbe wa kamati ya afya mkoa, wilaya, viongozi wa dini.

"Rai yangu kwenu mkatoe ushirikiano katika mradi huu, kwa kuhamasisha wananchi kuhusiana na chanjo ya kuzuia milipuko ya magonjwa yanayosababishwa na kutokupata chanjo ikiwamo chanjo za kawaida za watoto wenye umri chini ya miaka mitano na chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa shingo ya kizazi,"alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Girl Effect Tanzania, Khalila Mbowe, alisema mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne, ulianza mwishoni mwa mwaka jana ambalo utajumuisha wilaya za Monduli na Arumeru pamoja na Mkoa wa Shinyanga.

Alisema lengo la mradi ni kusaidia serikali katika kuongeza hamasa kwa jamii, ili watambue umuhimu wa chanjo hizo na kuhakikisha wanawafikia wasichana waliojifungua wakiwa na umri mdogo, pamoja na kutatua tatizo la kijinsia linalokwamisha matumizi ya chanjo kwao.

"Mradi utafanyika katika mikoa tofauti ila kwa kuanzia tumeanza na Arusha na Shinyanga na mwakani tutafikia mikoa tisa.

Alisema: "Kupitia mradi huu, tunatarajia kuongeza matumizi ya chanjo kwa watoto chini ya miaka miwili, kuongeza matumizi ya chanjo ya HPV kwa wasichana wa miaka 14 ili kuwakinga na saratani ya shingo ya uzazi na kuboresha tabia za ufuatiliaji wa mambo ya kiafya katika jamii."

## SBT, TEMDO wabuni mtambo wa kuzalisha sukari kwa wingi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

BODI ya Sukari Tanzania (SBT), kwa kushirikiana na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO), imebuni mitambo ya kisasa ya kuzalisha sukari kwa wingi utakaowasaidia wakulima na wafanyabiashara kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa hiyo hapa nchini.

Kutokana na sekta ya viwanda kuwa ni kiungo muhimu kwa ukuzaji wa uchumi wa taifa, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alifanya ziara TEMDO kuangalia ubunifu wa mitambo ya kilimo itakayosaidia kukuza biashara ya sukari.

Akizungumza jana katika ziara hiyo, Mavunde alisema kuna haja kutengeneza mashine na viwanda ambavyo vitasaidia wakulima kuongeza thamani ya mazao hayo.


"Lazima tufikie hatua ya kuongeza thamani ya bidhaa zetu watumishi mlioko chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara hakikisheni mnafanya kazi ya kutengeneza mitambo ya kuongeza thamani hasa mazao ya kilimo, uvuvi na mifugo kwa kuwa mmepewa jukumu kubwa na ninatamani kila siku mwendelee kuwa wabunifu wa vitu mbalimbali," alisema. Aidha, alisema mtambo huo umekamilika kwa muda muafaka kama walivyoahidi kwa lengo la kumtoa mkulima kutoka kwenye kilimo cha miwa mpaka kufikia kuwa mzalishaji wa sukari.

"Naomba mwendelee kuboresha teknolojia hizi kwa kuwa mna nafasi ya kuwasaidia wananchi, pia nakupongeza Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari kwa bunifu mlioufanya kwa kushirikiana na TEMDO kwa kutafuta namna ya kumsaidia mkulima kuondoka na tatizo la miwa kubaki shambani na kuharibuka," alisema Mavunde.

Alisema mtambo huo, utasaidia kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kwa mkulima ambaye analima miwa na yuko sehemu ambayo hawezi kupeleka bidhaa hiyo, katika kiwanda kikubwa.

Mkurugenzi wa SBT, Prof. Keneth Bengesi alisema lengo la kutengenezwa mashine hiyo ni kuhakikisha wanamsaidia mkulima kutoka kuuza mazao ya miwa ambayo bado hayajaongezewa thamani.

Mkurugenzi wa TEMDO, Prof. Frederick Kahimba,alisema wameanza kutengeneza mitambo mbalimbali itakayosaidia wananchi na watahakikisha matatizo yaliyoko yanatatuliwa kwa haraka.





# Familia yasimulia ndugu yao alivyopotea

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

FAMILIA ya Issa Hamis Issa (44) (Pichani) ambaye ni fundi magari mkazi wa Ndala Manispaa ya Shinyanga, mkoani Shinyanga imesimulia namna ndugu yao alivyopotea katika mazingira ya kutatanisha kwa takribani miezi mitatu sasa.

Issa anadaiwa kupotea miezi mitatu iliyopita akiwa na mwenzake aliyefahamika kwa jina la Perezi Bwee.

Akisimulia tukio hilo jana mdogo wake Issa, Hussein Hamis alisema ndugu yake huyo alipotea tangu Novemba mwaka jana akiwa na mwenzake (Bwee) na mpaka sasa hawajui walipo.

Alisema siku aliyopotea ndugu yake alitoka nyumbani majira ya asubuhi akiwaaga kuwa anakwenda kwenye shughuli zake za utengenezaji magari, lakini siku hiyo hadi jua linazama hakurudi nyumbani.

Alisema walipofuatilia kazini kwake wakaambiwa kuwa waliaga wanakwenda Mwanza na walipopiga simu zao zilikuwa hazipatikani.

Aliendelea kusimulia kuwa baada ya kaka yake kutopatikana kwenye simu pamoja na kumkosa kwa ndugu zake wote, walienda kutoa taarifa Kituo cha Polisi Shinyanga ili kuwasaidia kumpata, lakini mpaka sasa hakuna taarifa zozote wala hawajui aliko yeye na mwenzake.

"Baada ya kumkosa kaka yangu kwenye vituo vyote vya polisi pamoja na hospitali ili kujua huenda labda alipata ajali, ndipo ikabidi tupekue kwenye kitabu chake cha kumbukumbu (daily) na katika kupiga tukapata namba moja ikasema ndugu yetu anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mwanza,"alisema Hamisi.

Alisema walipofuatilia polisi Mwanza wakaambiwa hayupo kituoni hapo ndipo wakapiga tena ile namba wakaambiwa yupo Kituo cha Polisi Dodoma.

Akisimulia zaidi, alisema walipokwenda katika Kituo cha Polisi Dodoma wakaambiwa hayupo, ndipo wakapiga tena simu kwenye namba ile ile wakaambiwa yupo Kituo cha Polisi Dar es Salaam.

"Tulipoipigia tena ile namba tukauliza wamekamatwa kwa kosa gani? huyo mtu akatueleza kuwa wameiba gari la mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), lakini cha kushangaza huyo mtu hataki kujitambulisha yeye ni nani na akiongea kidogo anakata simu," alisema.

Alisimulia kuwa wakarudi tena Kituo cha Polisi Shinyanga kufuatilia taarifa za ndugu yao, wakaambiwa bado hawajampata kwamba wanaendelea kumtafuta na akipatikana watapewa taarifa.



Alisema kuwa ndugu yake ana watoto wawili, mmoja ana miaka sita na mwingine mwaka mmoja, hivyo analiomba Jeshi la Polisi liwasaidie kumtafuta kaka yake ili wajue mahali alipo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kuwepo kwa taarifa za kupotea kwa Issa Hamis Issa na kusema bado wanaendelea kumtafuta.



Baadhi ya wakulima na wafugaji wakishiriki kwenye ujenzi wa chumba kimoja cha darasa la wanafunzi wa shule ya awali kwenye Kijiji cha Kashanda, kata ya Nyakahanga, wilayani Karagwe, mkoani Kagera hivi karibuni. **PICHA: DANIEL LIMBE**

# Serikali yawapatia maofisa ugani pikipiki 230 kuimarisha kilimo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imetoa pikipiki 230 kwa maofisa kilimo katika halmashauri za Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kuwafikia wakulima katika maeneo yao ili kuimarisha shughuli za kilimo.

Hatua hiyo imeelezwa kuwa itasaidia kuleta tija katika kufanikisha kilimo bora na chenye tija ili kuongeza upatikanaji wa chakula cha uhakika.

Akizungumza wakati wa kukabidhi pikipiki hizo kwa wakurugenzi wa halmashauri mkoani Mwanza juzi, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Martine Shigela ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Geita aliwataka maofisa hao kuboresha kilimo ili kiwe cha kibiashara.

Shigela alisema serikali imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa maofisa ugani hao pamoja na maslahi yao na kwamba yanahitajika mabadiliko makubwa katika kilimo mkoani humo na nchini. "Sasa tuache kulima kwa mazoea, tulime kibiashara tujiwekee malengo ya kama ni mtaji umeweka kiasi gani na una faida kiasi gani hii itasaidia kumuinua mkulima mwenyewe na taifa litakuwa na chakula cha kutosha zaidi," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana aliwataka maofisa ugani kuhakikisha wanawafikia wakulima na kuwatatulia matatizo mbalimbali wanayokabiliana nayo ili kusaidia upatikanaji wa chakula cha uhakika nchini.

Alisema mkoa huo una maofisa ugani 269 wanaohudumia halmashauri nane za mkoa huo na awali zilitolewa pikipiki 30 kupitia bodi ya pamba hivyo kufanya kufikia idadi ya pikipiki 260.

# Atoa msaada wa katiba ya chama kwa makatibu kata CCM

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapindizi (CCM), Emmanuel Silanga ametoa msaada wa vitabu vya kanuni na katiba za chama hicho kwa makatibu wa kata za CCM mkoani hapa.

Pia ametumia fursa hiyo kuiomba serikali kuondoa marufuku ya usafiri wa gari ndogo katika kusafirisha abiria maarufu kama mchomoko.

Alitoa ombi hilo wakati wa maadhimisho ya miaka 46 ya kuzaliwa kwa CCM ambapo mkoani Simiyu yalifanyika viwanja vya Madeko wilayani Maswa.

Alisema marufuku hiyo imekuwa kikwazo kwa maendeleo ya wananchi wa mkoa huo wakiwemo vijana ambao wengi walichukua mikopo ili kufanya biashara hiyo ya usafirishaji.

Kutokana na hilo, Silanga ametaka kuwepo kwa kanuni ambazo zitasimamia usafiri huo ili kudhibiti ajali badala ya kuendelea kuzipiga marufuku.

"Mimi kama kiongozi wa chama nina jukumu kubwa la kuhakikisha viongozi wa chama wanajua kanuni na misingi ya chama chetu, hivyo nitatoa kanuni na katiba za chama kwa makatibu wote wa kata kwa mkoa huu," alisema Silanga na kuongeza:

"Chama chetu ni kikubwa kimetimiza miaka 46 Sasa. Najua tumefanya uchaguzi na umemalizika, kilichopo sasa ni kufanya kazi ya kuwatumikia Watanzania na wanaCCM wote kwa ujumla, hatuhitaji kuona tena kunakuwa na makundi ndani ya chama."

Kadhalika, alisema katika Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu atasaidia ufungwaji wa feni tano katika ukumbi mkubwa wa CCM uliopo wilayani humo, ili wanaCCM wanaotumia ukumbi huo wafanye vikao vya chama katika hali tulivu.

Kuhusu michomoko, Silanga alisema usafiri huo uliopigwa marufuku Julai 13, mwaka huu umekuwa ukiondoa vijana wengi kukaa vijiweni bila kushiriki shughuli za uzalishaji mali.

"Kuna namna Serikali inaweza kufanya jambo usafiri huu ukarejea lakini, kukawepo kanuni ambazo zitasimamia bila kuleta athari. Vijana wengi wamejiajiri kupitia sekta hii muhimu hivyo, kuendelea kwa marufuku ni kurejesha umasikini.

"Kwa sasa Simiyu tu ndiyo mchomoko zimezuiwa huku maeneo mengi zikiendelea, nadhani umefika wakati sasa tuliangalie hili," alisema Silanga.

Katibu wa CCM Mkoa wa Simiyu, Mohamed Ally akizungumza katika maadhimisho hayo aliwataka Watanzania na wananchi wa Simiyu kuacha kuwasikiliza watu wasiokuwa na hoja za msingi.




Ukurasa 12

**Ngawaiya: Upinzani ni kioo serikali ikitumie sasa kujitazama**



Ukurasa 13

Ndivyo Chongolo alivyowapa raha wanachama, wananchi



Ukurasa 14

**Papa Francis; aiamsha dunia inayosahau mateso Sudan Kusini, Congo**



## VYAMA KUTANDAZA MIKEKA

# Viache kulaumu, kulalamika vije na jibu kutumia rasilimali kimaendeleo

**Na Dk. Felician B. Kilahama**

KILA chenye mwanzo kina mwisho, yanadhihirika kwa sasa maana yale yaliyojiri katika ulingo wa siasa kwa miaka saba yamebadilika, ni ruhusa ya mikutano ya kisiasa.

Mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa iliyozuiliwa imerejeshwa kuashiria 'zuio' limefikia mwisho, kwa hali hiyo, 'hakuna lisilowezekana chini ya jua' hivyo tumshukuru Mungu kwa yote na kuiombea nchi yetu.

Vyama vya siasa vilikuwa vimekunja 'mikeka' sasa vinaitandaza rasmi ni hatua inayowezesha kutekeleza mambo mema kwa taifa hili kwa amani, maridhiano na upendo.

Aidha, ni jambo la kufurahisha kuwepo na utashi mkubwa wa kisiasa wa namna ambayo Tanzania imezingatia ili kuimarisha demokrasia na kwa maslahi ya wote.

Kwa muda mrefu CCM imeongoza nchi uwepo wa vyama vingi katika siasa za Tanzania ni dalili tosha kwamba haitatawala au kuongoza nchi au dola milele.

Tusemeje juu ya hali hiyo? Ni kwamba sasa kumekucha na dalili za kuashiria kwamba mzinga uliosheheni nyuki ulikuwa umefunikwa sasa mfuniko umeondolewa nyuki wametawanyika kila mahali wakitafuta chavua ili kutengeneza asali iliyosheheni utamu.

Lipo swali 2025 wananchi watarajie kupata asali iliyo-tamu zaidi au kitu gani baada ya nyuki kuondoka kwenye mzinga? Hapa ndipo, ilipojificha siri ya mafanikio kwa kila chama cha siasa.

Wakati Tanganyika au Tanzania Bara, inapata Uhuru Desemba 9, 1961 kilikuwepo Chama cha Tanganyika African National Union (TANU), wakati huo Zanzibar ilikuwapo na Afro-Shiraz na hatimaye kujitawala baada ya Mapinduzi yaliyofanyika Januari 12, 1964.

Haikuchukua muda mrefu, Serikali ya 'Tanganyika' iliyokuwa inaongozwa na TANU na ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Afro-Shiraz zikaungana Aprili 26, 1964 na kuanzisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivyo, kukawepo utawala wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar ikabaki na utawala wake wa ndani chini ya Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikawa inasimamia shughuli zote zilizokubaliwa na pande mbili kuwa za Muungano; lakini pia kushughulikia masuala yote yanayohusu iliyokuwa Tanganyika.

Hata hivyo, vyama hivyo viwili TANU na Afro-Shiraz, viliendelea kusimamia serikali hadi ilipozaliwa CCM Februari 5, 1977 baada ya kuunganishwa.



Huduma kama matibabu ni kitendawili kigumu, vyama pinzani visaidie mikakati na mbinu za kubadilisha hali duni kuwa bora. **PICHA: MTANDAO**

Baada ya hapo sera na siasa, vikawa vyombo vinavyosimamiwa na chama kimoja CCM Bara na Zanzibar hadi tulipoingia mfumo wa vyama vingi Aprili 28, 1992, ni baada ya kuridhia mfumo huo kichama na kisheria.

### KUJISAHAU

Kwa upande wa CCM, wakati mwingine, kumekuwepo na kujisahau na mambo yakawa hayaendi ipasavyo. Pengine, Mwenyekiti wa CCM ambaye ni Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan, mpaka kufikia uamzi huu wa kuruhusu mikutano ya vyama pinzani katika ulingo wa siasa, inawezekana hafurahishwi na hali hiyo.

Ili chama anachokiongoza kiwe msatari wa mbele, kinahitaji kuamshwa ili kutimiza wajibu wake ipasavyo kinyume chake kitajilaumu chenywe.

Kufika 2025 CCM itakuwa ina takriban miaka 50 huu siyo umri mdogo. Watanzania waliozaliwa wakati huo sasa ni watu wazima, inawezekana baadhi yao ni viongozi ndani ya chama.

Hivyo, ni kipindi kirefu kinatosha kwa chama kujipima na kujitathmini ipasavyo, maana ni takribani miongo mitatu tangu Tanzania iingie mfumo wa vyama vingi; kwa kipindi hicho lipo swali watu wamefanikisha na kujifunza nini?

### TUNAJIFUNZA NINI?

Hakuna majibu kwa swali hili lakini ni vizuri Watanzania wakatafakari kwa kina kuhusu jambo hilo muhimu.

Yawezekana moja ya mafanikio ni uwepo wa demokrasia na uhuru wa kufanya mambo. Zaidi ya hapo ni kujiuliza demokrasia maana yake nini, inaanzia na kuishia wapi au mambo ni hivyohivyo ili mradi baadhi ya watu wafurahi na mambo yaende? Tena hakuna uvunjaji wa sheria za nchi na kanuni zake?

Itakumbukwa ni zaidi ya miaka 60 tangu Uhuru ni kipindi ambacho nchi kama China sasa ni mataifa yenye nguvu kiuchumi na tishio duniani.

Historia inaonyesha kuwa wakati Tanzania inapata uhuru Wachina hawakuwa na nguvu kama walizonazo sasa je, wamefanyaje au ni mbinu gani walizotumia hadi kufikia hapo walipo?

INAENDELEA UK. 12

RUHUSA YA MIKUTANO

# Ngawaiya: Upinzani ni kioo serikali ikitumie sasa kujitazama

**Na Sabato Kasika**

TANGAZO la kuondoa zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, leo linatimiza siku 37, huku baadhi ya wanasiasa wa vyama vya upinzani waliokuwa uhamishoni wakiwa wamerejea nyumbani na wengine wako mbioni.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Tundu Lissu, ni mmoja wao, alikuwa anaishi Ubelgiji karudi Tanzania Januari 25 mwezi uliopita.

Kuruhusiwa kwa mikutano hiyo kumeendelea kuwaibua wadau, mitazamo na fikra mbalimbali kurejea uamuzi huo wa Rais Samia Suluhu Hassan, anaoutoa Januari 3 mwaka huu.

Miongoni mwa wadau hao, ni Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), inayomsifia Rais kwa kufanya uamuzi mgumu bila kusikia minong'ono na kelele za wasiotaka utawala wa vyama, vingi ikisema ni ushindi kwa Samia.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo ya jijini Dar es Salaam, Thomas Ngawaiya anaiambia Nipashe kuwa Rais amesimama kwa miguu yake, na kwamba kama kiongozi wa nchi aliyekomaa kisiasa ameona mapungufu yaliyokuwa kwenye katazo hilo na kuyasahihisha.

"Amefanya hivyo bila kujali minong'ono, anasema hapana, hatuwezi kuishi kwa kuogopana na kutaka vyama vingi virudi, kwani kwa miaka takribani saba ni kama havikuwepo.Amefanya jambo la kijasiri," anasifu Ngawaiya.

Anafafanua kuwa uamuzi wa Rais ni faida kwa nchi na kwa serikali, kwa maelezo kwamba, vyama mbadala ni kama kioo kinachosaidia kuona kasoro na kuzirekebisha.

"Vyama vya upinzani ni kioo cha kujiangalia kama taifa. Sisi CEGODETA tunaona ni faida kwa nchi na kwa demokrasia ya vyama vingi Tanzania. Huo ndio uongozi. Kama mtawala hataki kujitazama katika kioo ambacho ni mawazo mbadala, basi atakuwa na tatizo," anaeleza.

Kiongozi huyo anasema Rais anataka siasa za ushindani, ili hata mtu anapowania nafasi ashinde kihalali na si kupita bila kupingwa, na kwamba siasa za ushindani zitawaweka pembeni wale waliozoea ushindi wa kunyonga na wala si wa kuchinja na kuchuna kwa maana ya kufanyakazi kwa haki.



Thomas Ngawaiya (katikati), alipozungumzia ruhusa ya mikutano ya hadhara. Wengine ni wajumbe wa taasisi hiyo, Pricoline Mafoe (kulia) na Rahim Kibanda. **PICHA: SABATO KASIKA**

> Mkutano wa Lissu ulifanyika muda mfupi baada ya kutua siku hiyo akitokea uhamishoni nchini Ubelgiji nao pia unaandika historia.

"Kwa uamuzi huu wa Rais wa kurejesha demokrasia ya vyama vya siasa, nadhani haitakuwa vigumu kumtangaza mgombea wa upinzani kama atakuwa ameshinda katika uchaguzi, kwani miaka kadhaa iliyopita vyama vya upinzani vilichukuliwa kama maadui," anasema.

**ANGALIZO KWA VYAMA**

Mwenyekiti huyo anasema pamoja na mikutano ya hadhara, viongozi wa vyama vya siasa hawana budi kuzingatia kufanya siasa za kistaarabu, ili kuepusha msuguano kati yao na serikali.

"Watumie sheria ya vyama vingi vya siasa ya mwaka 1992, kuendesha shughuli zao za kisiasa, kwani inaelezea namna ya kufanya siasa kwa kurejea mwongozo," anasema.

Anaongeza kuwa kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria, hakuna mwanasiasa anayetafuta uongozi kwa kumchafua mwenzake na kuwashauri wanasiasa kuachana na mihemko ya kisiasa.

"Kufunguliwa kwa mikutano ya hadhara sasa kumeenda kuwafikirisha wanasiasa kuanza kujipanga upya namna ya kujibu hoja zitakazoelekezwa kwao katika mazingira ya kujenga hoja muhimu kwa taifa," anasema.

Ngawaiya anasema, iwapo wanasiasa watajenga hoja zenye mashiko kwa taifa, kuna uhakika hakutakuwa mmoja atakayefungua kinywa kwa matusi bali kukosoa na kushauri kistaarabu.

Anasema CEGODETA wadau wakuu wa utawala bora, wamefurahia hatua ya kuruhusu mikutano ya hadhara na kuongeza kuwa taifa linajengwa na Watanzania wote, bila kuegemea kwenye itikadi za vyama vya siasa.

"Rais amewahi kusema, kwenye kujenga Tanzania bora anatamani kujenga jamii yenye maridhiano na maelewano, umoja pasipo kujali tofauti zetu za kisiasa, kidini, kikabila na nyingine zote," anakumbusha.

Katika ufafanuzi, anasema Rais hakuishia hapo, bali alibainisha kuwa hilo litawezekana kwa kujenga jamii inayopata haki sawa mbele ya sheria, isiyobaguana na inayotoa fursa sawa za kiuchumi kwa wote.

"Anawaambia Watanzania kuwa anaamini maridhiano hayawezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia. Kauli hiyo inaendelea kupokelewa na wapenda maridhiano,"anasema.

Januari 3 mwaka huu, imeweka alama kwa vyama vya upinzani vitaikumbuka, kwani ndio ambayo Rais Samia alitangaza kuondoa zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, huku Chama cha Wananchi (CUF) kikiwa cha kwanza kufungua pazia la mikutano hiyo.

CUF ilifanya mkutano Januari 9, katika viwanja vya Bakhresa Manzese Dar es Salaam ulioandaliwa na chama hicho Wilaya ya Kinondoni, na kuhutubiwa ma Mwenyekiti wa chama taifa, Profesa Ibrahim Lipumba.

Baada ya CUF, CHADEMA nao wakazindua mkutano Januari 21 mwaka huu, jijini Mwanza ukihutubiwa na Mwenyekiti wa Taifa, Freema Mbowe, na kufuatiwa na mingine iliyofanyika Dar es Salaam, Mwembe Yanga, akirindima Makamu Mwenyekiti Lissu ,aidha, mingine imeendelea kufanyika Musoma na Tarime.

Mkutano wa Lissu ulifanyika muda mfupi baada ya kutua siku hiyo akitokea uhamishoni nchini Ubelgiji nao pia unaandika historia.

Wakati Lissu akiwa amerejea, mwanachama mwingine wa CHADEMA Godbless Lema, naye ametangaza kuwa yuko mbioni, ambapo taarifa zake zilizopo katika mitandao ya kijamii zinaelezea kuwa atatua Machi mosi mwaka huu.

Taarifa hizo zinaelezea kuwa atatua katika Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na kwenda moja kwa moja katika mkutano wa hadhara utakaofanyika jijini Arusha, ambako amewahi kuwa mbunge.

## Viache kulaumu, kulalamika vije na jibu kutumia rasilimali kimaendeleo

**INATOKA UK. 11**

Ni nguvu ya demokrasia au kuna 'siri' ya mafanikio yao zaidi ya dhana hiyo? Kwa upande wa Tanzania ndani ya kipindi hicho cha miaka 60 bado tunahangaikia huduma muhimu za kijamii ukiachilia mbali kuhangaikia uchumi na ujenzi wa viwanda.

**TUMESHINDA VITA?**

Wakati tumepata uhuru tulitangaza vita dhidi ya maadui maradhi, ujinga na umaskini. Hata hivyo, ukawa msisitizo kuwa ili kupambana sawasawa tunahitaji miundombinu imara ya barabara na kuwa na vyanzo vya uhakika vya nishati pamoja na kuendeleza kilimo chetu ili tupate uhakika wa kupata mazao ya chakula na biashara.

Katika vita ya kuondoa maadui hao watatu pia inaendana na kuongeza nguvu katika huduma za maji, elimu na afya. Hivyo kujenga na kuweka miundombinu imara katika sekta hizo hakukwepeki pamoja na kuwepo siasa safi na uongozi bora, pamoja na rasilimali ardhi na watu,wataalam na juhudi za kutosha.

Tukijitathmini tulikotoka, tulipo na tunakoelekea naweza kusema tumethubutu kwa kiasi fulani lakini kazi bado kubwa. Kusema kweli, kama siyo vita ya 'Iddi Amini wa Uganda' na kusababisha taifa kutumia rasilimali au fedha nyingi, vifaa na nguvukazi bila kutarajia, pengine Tanzania iungekuwa imefanya mengi zaidi.

Miaka ya 1970 ilikuwa lijengwe bwawa-kubwa la kuzalisha umeme kwenye eneo la 'Stigler's Gorge', Mto Rufiji. Hata hivyo, kutokana na athari za kivita katika uchumi ikawa imeshindikana. Pamoja na hayo baada ya vita Tanzania ilielekeza nguvu zake katika 'ukombozi wa mataifa' mengine ya Africa yaliyokuwa chini ya tawala za kibeberu. Kwa hali hiyo ikawa imepungukiwa uwezo wa kushughulikia masuala ya ndani ya nchi ikiwemo kupambana na maadui waliokuwa wametangazwa rasmi kitaifa.

**TUANZE SASA**

Kiuhalisia huduma za kijamii na masuala ya kiuchumi bado ni mahangaiko makubwa. Kwa mtazamo huo, CCM upinzani kuweni makini katika kuiwezesha Tanzania kufikia malengo muhimu ya kuwaletea maendeleo-endelevu wote haraka iwezekanavyo.

Malumbano ya kisiasa na kisera yalenge kuinua hali za maisha kwa wote na isiwe kuwaneemesha wachache wakati walio wengi wanateseka ndani ya nchi yao. Vyama pinzani visiwe ni vya kulaumu na kulalamika bali vije na 'hoja za msingi' nini kifanyike au kitakachofanyika kwa lengo la kutumia rasilimali kwa faida ya wote.

# Ndivyo Chongolo alivyowapa raha wanachama, wananchi

**Na Mary Geofrey,** aliyekuwa MOROGORO



Katibu Mkuu, Daniel Chongolo, akisikiliza na kutafutia majibu kero za maji wakati wa ziara yake Morogoro. **PICHA: MARY GEOFREY**

KATIBU Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, anahitimisha ziara mkoani Morogoro, akitatua kero zinazoibuliwa na wananchi na kutoa maelekezo kwa watendeji na wanasiasa wakiwamo mawaziri kumaliza changamoto zinazolalamikiwa.

Anakutana na kero vijijini hadi mikoani katika sekta za maji, umeme, barabara, afya, elimu, ardhi na kilimo, kwenye ziara ambayo anaongozana na Katibu wa Uenezi, Sophia Mjema na Katibu wa Oganaizesheni, Issa Gavu, kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM na uhai wa chama, kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Katibu baada ya kusikiliza kero anazokutana nazo, anawasimamisha watendaji wa serikali wakiwamo wa vijiji, kata, wilaya, mkoa na wizara kutoa maelezo.

"CCM ndiyo yenye dhamana ya kuongoza nchini, ndiye mmiliki wa duka, tuna haki ya kuhoji, kuagiza na kuchukua hatua, kwenye mambo ambayo hayaendi sawa," anawaeleza viongozi na wanachama na wananchi.

Akiwa kijijini Mikese, anakuta kituo cha afya cha Mikese, ambacho baadhi ya majengo yamekaa zaidi ya miaka mitatu bila kutumika kwa kukosa vifaa licha ya kukamilika.

Anachukizwa na hali hiyo na kuihoji Halmashauri ya Morogoro Vijijini, ambayo imeshindwa kutumia milioni 50 fedha za ndani, kununua vifaa vichache ili jengo la wazazi lianze kutoa huduma, wakisubiri vifaa kutoka serikalini.

Katibu Mkuu anashangazwa na halmashauri hiyo, kuwa na akiba ya bilioni 2.5 kwenye bajeti ya mwaka wa fedha uliopita na kusema.

"Hatuwezi kwenda namna hii, nitazungumza na Waziri wa TAMISEMI aje mwenyewe hapa ndani ya siku 14, aone fedha zilizowekwa hapa kwa ajili ya kujenga majengo haya lakini hayatumiki, inakuwaje"?

Hata tukiwaleta watumishi wa afya waliopangwa hapa nadhani wanatushangaa maana hawana kazi ya kufanya, madaktari nao hawana kazi wanatamani vifaa, anasema Chongolo.

"Na sisi tukija hapa tunasema kidumu Chama Cha Mapinduzi, kitadumu kama mambo yatanyooka, kama wenyewe tunajihujumu, haiwezekani ....."

### BARABARA KUSUASUA

Akiwa Ifakara wilayani Kilombero, ujenzi wa barabara ya Kidatu hadi Ifakara yenye urefu wa Kilomita 66.9 kwa kiwango cha lami, anaambiwa umedorora.

Anamuagiza Meneja wa Wakala waTaifa wa Barabara (TANROADS), Morogoro Lazack Kyamba, kumsimamia kikamilifu mkandarasi ifikapo Oktoba 15 mwaka huu, awe amemaliza.

Anaeleza kuwa fedha zilishatengwa na kuwaonya wasimamizi watakao kaidi maelekezo hayo ya chama.

> Hatuwezi kwenda namna hii, nitazungumza na Waziri wa TAMISEMI aje mwenyewe hapa ndani ya siku 14, aone fedha zilizowekwa hapa kwa ajili ya kujenga majengo haya lakini hayatumiki, inakuwaje"?

Akiwa katika Kijiji cha Melela, wilayani Mvomero, wananchi wanaibua kero ya kutolipwa fidia ya mashamba 2005 yaliyovamiwa na tembo.

Katika uvamizi huo, anaelezwa kuwa, wanavijiji 30 walipoteza maisha, na kusema changamoto haijibiwi kwa maneno mengi.

"Kama tembo walivamia maeneo ya watu, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana au watendaji wa wizara na kuna mamlaka zake zilizopewa majukumu, ndani ya siku saba wafike hapa kuwaona wananchi," anaagiza.

"Tembo wamekula mazao, watu walipwe fidia, kinachotakiwa fedha ilipwe kwa walioharibiwa mashamba yao, waje hapa mpate haki yenu."

### VIJIJI 68 GIZANI

Chongolo akiwa nyumbani kwa Katibu wa Shina namba 10 la chama hicho, Zainabu Ajili Kijiji cha Dumila Juu, anasalimiwa kwa kilio cha wananchi wa vijiji 68 kukosa umeme.

Aidha, wanalalamikia kuunganishiwa kwa Sh. 310,000 badala ya Sh. 27,000 iliyopangwa na serikali kwa maeneo ya vijijini.

Anawaahidi wananchi hao kuwa, Aprili mwaka huu, ataongozana na Waziri wa Nishati, January Makamba, kuwasha umeme katika vijiji vyote vya wilaya hiyo ambavyo havina huduma ilihali serikali imetoa fedha za kuwawekea umeme.

Chongolo anamtaka Meneja wa TANESCO, Fadhili Chilombe, kujibu kero hiyo. Akijibu anasema tatizo limetokana na kukosekana mawasiliano sahihi hapo awali.

"Kulikuwa kuna tatizo la mawasiliano ndio sababu ya kutozwa kiasi hicho, lakini kuanzia sasa watatozwa Sh. 27,000 badala ya 310,000."

### KUPUNJWA MIWA

Kero ya wakulima wa miwa kupunjwa malipo ya utamu wa miwa na kiwanda cha Sukari cha Kilombero, inaibuka akiwa wilayani Kilombero.

Katibu CCM Tawi la Sanje- Kidatu, Timotheo Kihanji, anawasilisha kero hiyo, kwa niaba ya wakulima ,wanaodai kupunjwa kwa maelezo kuwa miwa haina utamu unaokubalika na kiwanda hicho.

Akijibu, Chongolo, anamwagiza Mkuu wa Mkoa huo, Fatma Mwasa, kukaa na Vyama Vya Ushirika wa Kilimo na Biashara (AMCOS), kuteua mkulima mmoja katika kila chama, kwenda kufundishwa namna wanavyopima utamu wa miwa kiwandani.

"Wakifundishwa na kufahamu namna kiwango cha utamu wa miwa unavyopimwa, watatoa elimu kwa wakulima wenzao na kupunguza malalamiko ," anasema.

### MAWAZIRI KITIMOTO

Licha ya majibu waliyotoa kwa wananchi wakiwa katika vitongoji, vijiji na maeneo mbalimbali ya mkoa huo, Chongolo anaendelea kusaka suluhu ya kudumu kutoka kwa mawaziri.

Akihitimisha ziara yake mkoani Morogoro, anawaita mawaziri ambao wizara zao zinatakiwa kufuatilia, mfano TAMISEMI, Naibu Waziri, David Silinde, anatakiwa kujibu hoja ya mgawanyo wa walimu kwa usawa katika shule zote za serikali nchini, baada ya Chongolo kulalamikiwa kuwapo kwa upungufu wa walimu vijijini.

Silinde anasema baada ya agizo la Chongolo, tayari wameshatoa barua 545 za uhamisho kwa walimu wa mkoa huo na kutenga Sh. milioni 607 kwa ajili ya kazi hiyo.

"Tangu umetoa agizo la uhamisho, ndani ya siku saba tayari tumeanza kuwahamishia walimu katika shule ambazo hakuna walimu wa kutosha ikiwa ni awamu ya kwanza," anasema Silinde.

Kuhusu Shule ya Msingi Ngerengere, ambayo ilikuwa haijakamilika, anasema wamepokea maelekezo na Shilingi milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha ili wanafunzi waanze kusoma. Zimetengwa.

Akijibu vifaa vya matibabu katika zahanati na vituo vya afya mkoani humo, anasema serikali imetenga bilioni 95.7 na tayari vifaa vimeshaagizwa kwa ajili ya kufungwa na kutoa huduma ya matibabu.

"Kuhusu miradi ya barabara na mingine ya kimkakati ambayo imeshindwa kukamilika kwa wakati, Waziri wa TAMISEMI, Angela Kairuki, ataanza ziara wiki ijayo katika mkoa huu kwa ajili ya kuanza utekelezaji," anasisitiza.

### SHIDA YA MAJI

Chongolo anamtaka Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, kujibu hoja ya tatizo la kukosekana maji katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo ambayo yalilalamikiwa na wananchi katika ziara yake.

Maryprisca anasema, wizara inafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha wanawake wanapata huduma ya maji nchini ili kuokoa ndoa zao zilizopata shida kutokana na foleni ya kutafuta maji.

Anasema umbali wa kupata huduma ya maji hautakuwa zaidi ya mita 400 katika maeneo yote nchini.

PAPA FRANCIS

# Aiamsha dunia inayosahau mateso Sudan Kusini, Congo

• Amewabeba Kiir, Machar 2019 aliwabusu miguuni
• Aacha nukuu: "Toeni mikono yenu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo! Kaeni mbali na Afrika! Acheni kuibana pumzi Afrika, si mgodi wala ardhi ya kuporwa hivi."

**Na Gaudensia Mngumi**

NDIVYO PAPA Francis anavyoguswa na Congo na Sudan Kusini, akiumizwa na mateso ya mamilioni ya watu ambao huchomwa visu, hukatwa mapanga , kupigwa risasi na kuuliwa kila wakati.

Licha ya hali ya hofu kiusalama Papa, anaanza mwaka 2023 kwa safari ya DRC na Sudan Kusini kuiamsha dunia hasa mataifa yenye uwezo na nguvu kiuchumi kuwa yamesahau mzozo wa Sudan Kusini na DRC.

Kiongozi huyu wa Kanisa Katoliki Duniani, ana uchungu na Sudan Kusini na kwa mara ya kwanza Papa Francis anahimiza amani nchini humo na kuwahurumia maskini.

Anachofanya mwaka 2019, wakati wa mkutano wa amani huko Vatican, Francis anapiga magoti mbele ya viongozi wa Sudan na kuwabusu miguu Rais Salva Kiir na makamu wake Dk. Riek Machar.

Papa, hajakurupuka alikuwa akipanga kuzuru Sudan Kusini kwa miaka mingi lakini alicheleweshwa na hofu ya usalama, lakini hata hivyo amewafikishia ujumbe Kiir na Machar alipokutana nao nyumbani kwao.

Mwaka 2011, Sudan Kusini ilikuwa nchi mpya zaidi duniani baada ya kujitenga na mbabe Sudan wakati huo ikiongozwa na Rais Omar al- Bashir.

Furaha ya taifa jipya ilikuwa ya muda mfupi, kwani nchi hiyo imetumbukia kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe na njaa kwa miaka yote.

Sasa, Papa Francis anajaribu kuongeza umakini wa kimataifa kwa Sudan Kusini anapoanza safari ya siku tatu, iliyoanza Ijumaa Februari 3, nchini humo kama sehemu ya kutimiza "hija ya amani duniani."

Safari ya Papa, pamoja na Askofu Mkuu wa Canterbury, ambaye ndiye Mkuu wa Kanisa la Anglikana Justin Welby, na Msimamizi wa Baraza Kuu la Amani Iain Greenshield, ni wahusika wakuu kwenye masuala ya usuluhishi na amani.

Aidha, akiwa na Papa anajikita katika kuongeza ufahamu kuhusu mzozo ambao umesababisha vifo vya zaidi ya watu 400,000 nchini Sudan.

Wakristo wengi wa Sudan Kusini walijitenga na Sudan yenye Waislamu wengi mwaka 2011, lakini licha ya kutarajia furaha na amani, ipo kwenye mzozo wa kisiasa na kikabila kati ya Rais Kiir na Makamu Dk.Machar. Ni vita vya kikabila kati ya Wadinka kabila la Kiir la Wanuer la Makamu .



Papa Francis alipotua DRC wiki iliyopita kuhimiza amani na kuacha vita vinavyoua maelfu ya watu. **PICHA: MTANDAO**

"Nchi hiyo inakabiliwa na masuala kadhaa kama ukimbizi wapo wakimbizi wa ndani milioni 2.2wakati watu milioni 2.3 wameikimbia nchi hiyo, kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa.



Papa Francis akiibusu miguu ya Rais Salva Kiir na Makamu wake Dk. Machar kuwasihi wapatane, waache vita na kuleta amani. **PICHA: MTANDAO**

### KWANINI SUDAN K?

Baada ya ziara ya mafanikio nchini DRC, Papa anawasili Juba, Sudan Kusini na kulakiwa na umati, taifa hilo lenye umri wa muongo mmoja halijawahi kumkaribisha kiongozi wa nchi za Magharibi wala mzito kama Papa katika ziara ya kiserikali.

Watu watatu mashuhuri ten wenye hekima Papa Francis, Askofu Mkuu Welby, na Greenshield wanalakiwa na maelfu ya watu waliokuwa wakiimba na kupiga kelele kushereheekea ujio huo mkubwa.

Sudan Kusini yenye watu milioni 11, takriban milioni 6.0 ni Wakatoliki, katika enzi ya ukoloni, wamishenari wa Kikristo nchini Sudan waligawanywa na mto Nile, na Wakatoliki na Waanglikana walilazimishwa kuhubiri pande zinazopingana, kwa mujibu wa gazeti la New York Times.

Francis aliunganishwa tena na Rais Kiir, anayeliongoza taifa hilo tangu uhuru mwaka 2011, na Makamu wake, ambaye sasa amegeuka mpinzani Dk. Machar.

### VIFO VYAMKARIBISHA

Ni kama kusema ziara ya Papa ilikaribishwa na vifo, ni mapigano makali kati ya wafugaji na wanamgambo siku moja kabla ya kuwasili kwa Papa Francis yakikumbusha mzozo unaoendelea.

Katika mapigano hayo watu 27 wanafariki wakiwamo watoto watano, akiandika kwenye twitter, Welby anataja mauaji hayo kuwa ni "hadithi ambayo mara nyingi husikika kote Sudan Kusini."

Nchi hiyo inakabiliwa na masuala kadhaa kama ukimbizi wapo wakimbizi wa ndani milioni 2.2wakati watu milioni 2.3 wameikimbia nchi hiyo, kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa.

Mwaka jana, Sudan Kusini ilikuwa kinara wa ufisadi duniani kwa mujibu wa ripoti ya taasisi ya Transparency International.

Nchi hiyo inakabiliwa na ripoti kadhaa za uchunguzi zinazoonyesha jinsi mapato ya mafuta yenye thamani ya mabilioni ya dola yanavyotoweka na maofisa hawawezi kuelezea utajiri huo, linaripoti New York Times.

### PAPA DRC

Kwa nini Papa anatembelea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo? Jibu, kama Sudan Kusini, pia imekuwa ikikabiliana na mzozo. Zaidi ya makundi 120 ya waasi yamejifungia katika mzozo na serikali kwa miongo mitatu.

Kanisa Katoliki limekuwa na mkono wa kusimamia na kushauri serikali na kukemea uovu DRC, mwaka 2019, maaskofu na mapadri waliosimamia uchaguzi na matokeo yake ki kuchaguliwa Rais Felix Tshisekedi kuchukua uongozi.

Wakati wa ujio wake DRC ilitangaza kuwa sikukuu ya watu wote kuadhimisha ziara hiyo isiyo ya kawaida ya papa tena ya kwanza katika karibu miongo minne sasa. Umati mkubwa wa watu ulikusanyika katika mji mkuu, Kinshasa, kumpokea na kumtazama Papa Francis akfanya ibada ya misa kwenye uwanja wa wazi. Takriban nusu ya raia wa DRC ni Wakatoliki na kuwa taifa lenye Wakatoliki wengi zaidi barani Afrika.

### KUKEMEA UKOLONI

Wakati wa hotuba yake, Papa Francis analaani historia ya ukoloni wa Ulaya na unyonyaji wa rasilimali za Afrika, akieleza kuwa madini yana jukumu muhimu katika mapigano yanayoendelea sasa.

Mjumbe wa Vatican nchini DRC anasema safari ya Papa inalenga kukumbusha duniani kutopuuza mizozo ya miongo kadhaa. Anapigiwa makofi anaposema: "Mikononi mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo! Mikono mbali Afrika! Acheni kuisonga Afrika, si mgodi wa kuvuliwa nguo au ardhi ya kuporwa."

Taifa hilo pia limekuwa na makundi zaidi ya 100 yenye silaha yanayopigania udhibiti wa maeneo au kuyatumia kama ngome kushambulia nchi jirani kama vile Angola, Rwanda na Uganda, inaripoti Al Jazeera.



## Wafugaji waonywa kuchunga mifugo katika vyanzo vya maji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imewaonya wafugaji wa mifugo kuacha tabia ya kuchunga mifugo yao holela kwenye maeneo yaliyopandwa miti na vyanzo vya maji ili kusaidia kulinda mazingira.

Aidha, imesema inapanga kuanzisha operesheni ya kukamata mifugo yote ambayo itabainika kuzurura ovyo katika maeneo ya mjini ili kufanikisha mpango wa serikali wa kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Onyo hilo limetolewa na Ofisa Mazingira wa Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa upandaji miti katika eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Alisema tabia hiyo ya kuchunga mifugo kwenye maeneo hayo na kuiachia mifugo ikizurura hovyo mitaani, hawatavumilia na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kuwatoza faini ya Sh. 300,000.

Kimaro alisema halmashauri hiyo itaihakikisha mifugo ambayo inazurura na kuchungwa kwenye maeneo yasiyotakiwa inakamatwa na kutoa faini hiyo kutokana na kukaidi agizo hilo.

Hata hivyo, alizitaka taasisi na watu binafsi kuacha tabia ya kukata miti ovyo bila kibali cha kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji.

"Imegundulika kuwa taasisi na watu binafsi wanaokata miti hiyo walio wengi wanaharibu mazingira, hivyo Halmashauri ya Jiji inawaagiza wanaotaka kukata miti hiyo lazima sasa waombe kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Jiji" alisema.

Alisema kuwa kwa hivi sasa kuna mwitikio mkubwa wa wananchi wa kupanda miti kutokana na uhitaji mkubwa unaojitokeza.

# Wadau serikali mtandao kukutana kujadili matumizi TEHAMA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU 1,000 wa serikali mtandao wanatarajia kukutana jijini Arusha kwa ajili ya kuweka mikakati mbalimbali ya kukuza serikali mtandao nchini, kuwa na matumizi sahihi na salama ya TEHAMA kwenye taasisi za umma.

Akizungumza jana jijini hapa kuhusu kikao kazi cha tatu, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Mhandisi Benedict Ndomba, alisema kikao hicho kitafanyika kuanzia Februari 8 hadi 10, mwaka huu na kitafunguliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama.

Alisema wadau hao ni kutoka katika mashirika na taasisi za umma wakiwamo maofisa masuuli, wajumbe wa bodi, wakuu wa vitengo vya TEHAMA, maofisa rasilimali watu, maofisa mipango, maofisa mawasiliano, wahasibu pamoja na watumiaji wote wa mifumo ya TEHAMA serikalini.

"Kikao kazi cha tatu cha serikali mtandao kinaongozwa na kaulimbiu isemayo 'Mifumo jumuishi ya Tehama kwa utoaji huduma bora kwa umma', lengo ni kuboresha utendaji kazi katika taasisi hizo pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi,"alisema.

Alitaja baadhi ya mafanikio yatokanayo na eGA ni kusimamia uzingatiaji wa sera, sheria na miongozo ya serikali mtandao kwa taasisi za umma.

"Kuwezesha usanifu na ujenzi wa mifumo ya serikali mtandao ya kitaasisi na ya kisekta ili kuboresha utoaji huduma kwa umma, kuboresha na kuongeza mawanda ya kusimamia uendeshaji wa miundombinu shirikishi ya serikali mtandao,"alisema.

Alisema mamlaka imejipanga kuweka mwelekeo wa serikali mtandao katika miaka ijayo kwa kuandaa na kutekeleza mikakati madhubuti ili serikali mtandao ifikie kuwa na sehemu moja ambayo huduma mtandao zote zitakuwa zinapatikana.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy (kushoto waliokaa) akiwa pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Maji, Haji Nandule (kulia waliokaa) wakionyesha nyaraka baada ya kutiliana saini hati ya makubaliano ya kusimamia dirisha la utoaji mikopo kwa watekelezaji wa miradi ya maji nchini, wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa Sekta ya Maji, jijini Dodoma juzi. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (wa pili kushoto waliosimama) na Naibu wake, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto waliosimama). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali Benjamin Mkapa yasaini ushirikiano upasuaji moyo watoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa imesaini makubaliano ya ushirikiano wa kutoa huduma za upasuaji wa moyo kwa watoto na Shirika la Children Heart Charity Association la nchini Kuwait.

Awali hospitali hiyo ilikuwa inatibu watoto 400 kwa mwezi hivi sasa watakuwa na uwezo wa kutibu watoto 3,400.

Akizungumza wakati wa kutia saini makubaliano hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika alisema makubaliano hayo yameangazia maeneo makuu matatu.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni kugharamia watoto wenye matatizo yanayohitaji upasuaji wa moyo na kuwezesha vifaa tiba vinavyohitajika kwenye matibabu ya moyo.

Alisema eneo la tatu ni kuwajengea uwezo madaktari, wauguzi na wataalam wa huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo kwa Hospitali ya Benjamin Mkapa.

"Tunaishukuru sana Kuwait kwa kujitolea kutusaidia matibabu ya moyo kwa watoto wadogo,"alisema Dk. Chandika.

Alifafanua zaidi kuwa pamoja na utiaji saini tayari jopo la madaktari, wauguzi na wataalam wa huduma za matibabu ya moyo kutoka Kuwait wamewasili katika hospitali hiyo kutoa huduma za uchunguzi tangu Februari 3, mwaka huu watakuwepo hadi Februari 9 na wanatarajia kuwafanyia uchunguzi watoto 100 na kupatiwa matibabu.

Balozi wa Tanzania nchini Kuwait, Said Musa alisema ujio wa madaktari bingwa hapa nchini utasaidia kutoa huduma za moyo kwa watoto ikiwamo upasuaji.

Alisema anawashukuru Hospitali ya Benjamin Mkapa kutokana na ushirikiano waliotoa kwa madaktari hao na kuwataka waendelee kuwa na moyo wa utoaji matibabu ya moyo.

Dk. Faisal Al-Saied alisema wanaimani malengo wanayotarajia kuyafikia yatafanikiwa kwa sababu wamepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa uongozi wa hospitali hiyo.

Alisema jamii inapaswa ijitokeze kwa ajili ya kupata matibabu ya moyo kwa watoto wadogo hususani wale wanaohitaji upasuaji.



# Maonyesho ya teknolojia za madini kufanyika Chunya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kwa kushirikiana na baadhi ya taasisi imeandaa maonyesho ya teknolojia za madini na fursa za uwekezaji katika sekta hiyo ili kuongeza uzalishaji, mapato yatokanayo na shughuli za uchimbaji nchini.

Maonyesho hayo yanatarajiwa kufanyika katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya kwa siku tano kuanzia Machi 21 mpaka 25 mwaka huu ambapo wadau mbalimbali wa madini watashiriki.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake ambapo alisema maonyesho hayo yatafanyika kwa mara ya kwanza katika mkoa huo wa kimadini wa Chunya.

Aliwataja baadhi ya wadau watakaoshiriki kuwa ni wachimbaji, wafanyabiashara wa madini, taasisi za kifedha pamoja na wauzaji wa mitambo inayotumika kwenye uchimbaji.

Homera alisema maonyesho hayo yatasaidia kuongeza uzalishaji wa madini katika mkoa huo ambao alisema ni wa pili kwa uzalishaji wa madini baada ya kuanzishwa masoko ya madini ambayo yanakusanya takwimu.

"Tumemwalika Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko, aje atufungulie maonyesho haya, sasa tunategemea yeye ndiye atatutafutia mgeni mwingine, kuna uwezekano akaja kufungua Waziri Mkuu au Makamu wa Rais ama Rais mwenyewe," alisema Homera.

Alisema baada ya maonyesho hayo, uwekezaji kwenye sekta ya madini utaongezeka na wachimbaji watabadili mbinu za uchimbaji kwa kujifunza teknolojia mpya na za kisasa zitakazokuwa zinaonyeshwa.

Baadhi ya waandaaji wa maonyesho hayo walisema shughuli mbalimbali zitafanyika katika siku zote tano ikiwamo ziara kwenye maeneo mbalimbali ya uchimbaji.

Mmoja wa waandaaji hao, Thomas Richard, alisema wadau watatembelea migodi mbalimbali kwa lengo la kujifunza teknolojia zinazotumika kwenye uchimbaji pamoja na kushauri njia bora za uchimbaji.

Alisema wachimbaji wa madini watakaohudhuria watafundishwa teknolojia mbalimbali za uchimbaji ambazo ni rafiki kwenye mazingira.

"Tutatembelea pia masoko ya madini yaliyopo katika mkoa wa kimadini wa Chunya, tutaangalia namna shughuli za ununuzi zinavyofanyika, tutapita pia kwenye maeneo ya uchenjuaji ili tuone pia mbinu zinazotumika," alisema Richard.

Aliwataka wachimbaji kutoka katika maeneo mbalimbali kuhudhuria maonyesho hayo ili wajifunze teknolojia za kisasa ambazo zinatumika kwenye uchimbaji.

Naye George Lupenza alisema katika maonyesho hayo taasisi mbalimbali za kifedha zitakuwapo kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wachimbaji ambao watakuwa na uhitaji wa mitaji.

Baadhi ya wachimbaji wa dhahabu wilayani Chunya, waliishukuru serikali kwa kuanzisha maonyesho hayo wakieleza kuwa yatawasaidia kuboresha shughuli zao za uchimbaji.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji wa Dhahabu wilayani Chunya, Leonard Manyesha, alisema maeneo mengi ya wilaya hiyo wachimbaji wamekuwa wakitumia mbinu duni za uchimbaji hali ambayo inafanya uzalishaji kuwa mdogo.

Alisema baada ya maonyesho hayo wachimbaji wataboresha mbinu za uzalishaji kwa kuanza kutumia teknolojia za kisasa ambazo watajifunza kupitia maonyesho hayo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini humo juzi, kuhusu maandalizi ya maonyesho ya teknolojia za madini na uwekezaji katika sekta hiyo yatakayofanyika wilayani Chunya mwezi Machi mwaka huu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wapanda miti Hospitali ya Kanda kutunza mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMISHI wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, wameungana na wadau mbalimbali wa mazingira kupanda miti ya matunda na vivuli kuzunguka maeneo ya hospitali hiyo kwa lengo la kutunza mazingira.

Watumishi hao walipanda miti hiyo juzi kwa ajili ya kuwahamasisha wananchi pia kushiriki kupanda miti kwenye makazi yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alisema wamekuwa wakifanya kazi hiyo kila mwaka kama sehemu ya kuwahamasisha watumishi kutunza mazingira yanayowazunguka.

Vilevile alisema walihamasika kupanda miti hiyo kwa ajili ya kuungana na serikali ya mkoa huo kurejesha mazingira ya mkoa huo katika hali ya ukijani.

"Tunaamini kwamba wananchi walioTuona tukifanya kazi hii pia wamehamasika na wataenda pia kupanda majumbani mwao, hii miti ya vivuli inawasaidia wateja wetu wakati mwingine kupumzika hasa wakati wa jua kali," alisema DK. Mbwaji.

Baadhi ya watumishi wa hospitali hiyo walimshukuru Dk. Mbwaji kwa kuwahamasisha kushiriki kazi hiyo kwa maelezo kuwa linasaidia kuyafanya mazingira ya hospitali kuwa mazuri.

# H'shauri Mbeya kutumia bil.87/- shughuli za maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imepanga kutumia Sh. bilioni 87.5 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu wa Jiji la Mbeya, Ally Nnunduma, aliyasema hayo jana alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha ujao.

Alisema bajeti hiyo imeongezeka kwa zaidi ya Sh. bilioni moja ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/2023 na kwamba ongezeko hilo limetokana na ongezeko la shule moja ya msingi ya mchepuo wa Kiingereza.

Alisema vipaumbele vya halmashauri hiyo ni uboreshaji wa sekta ya elimu, afya na miundombinu ya masoko katika Jiji hilo ili kuhakikisha huduma za kijamii zinaboreshwa zaidi.

"Fedha hizi zitatokana na makusanyo ya ndani Sh.bilioni 19.23, ruzuku kutoka serikalini Sh. bilioni 1.022, ruzuku kutoka serikalini kwa ajili ya mishahara Sh. bilioni 55.57, miradi ya maendeleo Sh. bilioni 7.4, fedha za elimu bila malipo Sh. bilioni 3.11 na michango ya wananchi Sh. bilioni 1.21," alisema Nnunduma.

Meya wa Jiji hilo, Sheikh DorMohamed Issa, aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kushirikiana na wataalamu kuhakikisha bajeti hiyo inafanikiwa ili kufikia malengo ambayo yamewekwa.

Alisema moja kati ya vipaumbele muhimu vya kutekeleza ni kuhakikisha huduma za kijamiii zinaboreshwa na Jiji linafanyiwa usafi ili liendane na hadhi yake.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliishauri halmashauri hiyo kusimamia vizuri utekelezaji wa bajeti iliyopitishwa ili kuhakikisha wananchi wanahudumiwa vizuri.

Malisa aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kuzingatia asilimia 10 ya mapato ya ndani kutengwa kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuendana na sheria za nchi.

Vilevile aliwataka kuhakikisha asilimia 60 ya fedha zinazokusanywa zinarejeshwa kwenye jamii kwa ajili ya maendeleo na kwamba lazima wafuatilie miradi inayotekelezwa ili kujiridhisha.

"Lakini nawaomba sana mhakikishe asilimia 10 ya mapato ya ndani kinatengwa kwa ajili ya vikundi vya wajasiriamali na mhakikishe vinakopeshwa vikundi sahihi na kufuatilia urejeshaji wake," alisema Malisa.

Katika hatua nyingine Malisa aliwataka madiwani pamoja na wataalamu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kushirikiana kutoa elimu kwa wananchi ili watunze mazingira na vyanzo vya maji kwa kuhakikisha wanapanda miti.

Alisema tatizo la mabadiliko ya tabianchi linaloikumba dunia kwa sasa linasababishwa na uharibifu wa mazingira na hivyo akawataka kuhakikisha wanashiriki kurejesha uoto wa asili uliohariblwa katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Wakili Triphonia Kisiga, alisema halmashauri hiyo inaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani pamoja na ruzuku kutoka serikali kuu.

Alisema halmashauri hiyo ina mipango ya kuhakikisha inaongeza ukusanyaji wa mapato kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Alisema kwa sasa wametekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, vituo vya afya na zahanati pamoja na huduma zingine muhimu za kijamii.



## KIST yatakiwa kutumia fursa, kwenda na teknolojia mpya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, ameitaka Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST) kuitumia fursa iliopo katika mradi wa AHUMAIN ili kuenda sambamba na teknolojia mpya zinazoibuka ulimwenguni.

Alisema kutokana na kuibuka kwa teknolojia mpya mara kwa mara ulimwenguni ni vyema KIST ichangamkie fursa za miradi kama hiyo ili kufikia teknolojia ya kisasa, ambapo miongoni mwa njia za kufikia teknolojia hizo ni kuichangamkia fursa iliopo katika mradi wa huo utakaowawezesha Watanzania kujifunza teknolojia mpya na za kisasa.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua mradi huo kwa upande wa Afrika Mashariki, katika Chuo cha Mbweni Zanzibar, ambapo kwa Tanzania KIST na Chuo kikuu cha Ardhi, ndiyo vilivyo bahatika katika mradi huo.

Alieleza kuwa kupitia mradi huo KIST itakuwa na programu mbili mpya na za kisasa ikiwamo 'Human Intelligence' na 'Data Science' ambazo ni programu muhimu na zenye soko, lakini zitasaidia katika kufanikisha maendeleo ya teknolojia nchini.

Aidha, alisema mradi huo utawawezesha wananchi wa Afrika Mashariki kupata fursa ya kushiriki katika mafunzo yatakayotolewa ndani na nje ya nchi, hivyo amewataka wananchi kuichangamkia fursa hiyo. Mkuu wa KIST, Dk. Mahmoud Abdulwahab Alawi, alisema mradi huo umelenga kuhakikisha Tanzania inakwenda sambamba na teknolojia mpya ambazo zinaibuka katika mataifa ili maendeleo ya teknolojia kupatikana kwa haraka.

Alisema kuwa, maendeleo ya viwanda na teknolojia kwa ujumla, yanazidi kukua duniani, hivyo ni lazima nchi za Afrika zitafute fursa ya kuweza kupata maendeleo ya teknolojia, ikiwamo kushiriki katika miradi kama hii inayojumuisha taasisi mbalimbali ulimwenguni.

Mratibu wa Mradi KIST, Mkufunzi Ali Abdullah, alisema mradi huo unalenga kuipa uwezo kompyuta kufanya maamuzi ya kibinadamu yaliyosahihi na ya haraka, ili kufanikisha kazi kwa wakati na kuongeza uzalishaji wa bidhaa hasa viwandani.

Alisema mataifa yaliyoendelea yanapiga hatua kubwa katika maendeleo, kutokana na matumizi ya teknolojia za kisasa, hivyo ipo haja kwa nchi za Afrika kuitumia fursa hiyo kwa lengo la kukuza uzalishaji.



Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban (wa pili kushoto), akisisitiza jambo wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Maruhubi, Unguja jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yusuph Majid Nassor. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZBS yaagizwa kudhibiti ubora, kuimarisha uzalishaji bidhaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, ameitaka Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kudhibiti bidhaa zilizo chini ya viwango na kuimarisha uzalishaji wa ndani.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa bodi hiyo katika ofisi za ZBS Maruhubi, Omar aliwataka wajumbe wa bodi na uongozi kuhakikisha wanashirikiana kukamilisha majukumu yaliyomo katika mpango kazi wa taasisi ikiwamo ujenzi wa ofisi na maabara katika Kisiwa cha Pemba.

Aidha, aliipongeza bodi hiyo iliyoteuliwa kwa kipindi cha pili kwa kukamilisha ujenzi na upatikanaji wa jengo la ofisi na maabara za kisasa hali iliyoongeza ufanisi wa taasisi kwa wadau wake.

"Sitarajii kuona kunakuwa na mvutano baina ya bodi na 'management' (uongozi) bali natarajia mtaendelea kushirikiana kuleta mafanikio zaidi katika siku za usoni," alieleza Omar.

Aliwataka wajumbe wa bodi hiyo wanaotoka katika taasisi za serikali na binafsi kutambua kuwa wao ni sehemu ya ZBS hivyo wanapaswa kuwa mabalozi na kusaidia kuondoa matatizo pindi yanapojitokeza.

Alisema taasisi hiyo kukamilisha taratibu za kupata alama ya ithibati ya ubora inayotolewa na Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO) ili kuiongezea hadhi na thamani taasisi lakini alama ya ubora inayotoa.

Waziri huyo pia aliitaka ZBS kusimamia udhibiti wa ubora wa bidhaa za nguo, kanga na vitenge zinazoingia nchini ili kukipa uwezo Kiwanda cha Basra Textiles wa kushindana.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Khadija Saleh Abdalla, alisema kuwa wamejipanga kusimamia majukumu ya taasisi hiyo likiwamo la kukamilisha maandalizi ya mpango kazi pamoja na kuanza ujenzi katika eneo la viwanda Chamanangwe, Pemba.

Aliyataja maeneo mingine yatakayosimamiwa na bodi hiyo kuwa ni ujenzi wa eneo la ukaguzi wa magari na kuongeza idadi ya wajasiriamali wanaofikiwa ili kupatiwa alama ya ubora wa bidhaa wanazozalisha ili kuyafikia masoko makubwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yusuph Majid Nassor, alisema kuwa katika kipindi cha uhai wa bodi hiyo, ZBS imefanikisha ujenzi wa ofisi na kuanzisha maabara ikiwamo ya bidhaa za petroli na kwamba mchakato wa kuanzisha maabara na ofisi katika eneo la Chamanagwe umeanza.

Alisema kuwa katika kujenga uwezo wa kitaasisi na kuitambulisha kwa jamii, ZBS imelenga kuendeleza majukwaa ya majadiliano na makundi mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari kupitia taasisi zao.

# ZAWA, ZECO zatakiwa kutoa huduma za uhakika

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi, imeitaka Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), kuwapatia wananchi huduma za uhakika.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Yahya Rashid Abdalla, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa wizara.

Alisema ni lazima wizara kusimamia mambo muhimu ikiwamo upatikanaji wa huduma ya umeme na maji kwa wananchi na maeneo hayo yamekuwa yakilalamikiwa.

Aidha, alibainisha kuwa wananchi wengi wanakosa huduma ya maji ya uhakika na upatikanaji mdogo wa miundombinu ya umeme katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema ni lazima wizara kuyasimamia mambo hayo na miradi yote wanayoitekeleza ili kufanyika kwa wakati kwa lengo la kuwaondolea usumbufu wananchi na kufikia azma ya serikali ya kuwapelekea wananchi maendeleo.

Hata hivyo alilitaka ZECO kuhakikisha linafuatilia madeni hasa katika taasisi za serikali ili kuhakikisha huduma hiyo inaimarika mjini na vijijini.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa programu kwa wizara hiyo Julai hadi Desemba mwaka jana, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Shaaban Ali Othman, alisema kwa kipindi hicho wizara imekusanya Sh. bilioni 6.3 sawa na asilimia 120 ya Sh. milioni 5.2 ambazo zilipangwa kukusanywa.

Alisema wizara imevuka lengo la makusanyo hayo kutokana na kuimarika kwa udhibiti wa rasilimali za mchanga na uwapo wa uratibu mzuri wa rasilimali hizo pamoja na kuimarika kwa mfumo wa kielektroniki wa maombi ya vibali vya rasilimali zisizorejesheka.

Kuhusu Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), alisema imefanikiwa kurejesha huduma ya maji katika maeneo ya Unguja na Pemba baada ya ununuzi wa mashine mpya na kuziweka katika visima vilivyokuwa na hitilafu.

Alisema mashine 103 zimefungwa katika visima 100 vya Unguja na Pemba na kusababisha uzalishaji wa maji kuongezeka kutoka asilimia 63 hadi 65 kwa Unguja na asilimia 62 hadi 67 kwa Pemba na kufanya wastani wa asilimia 66 upatikanaji wa maji nchini.

Aidha, alisema ZAWA imefanikiwa kubadilisha mtandao wa mabomba chakavu pamoja na kupanua mtandao wa maji katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao huo, kwamba jumla ya mita 19,440 za mabomba zimelazwa kati ya hizo mita 9,660 Unguja na 9,780 kwa Pemba.

Alisema mamlaka hiyo imefanikiwa kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma ya maji kwa asilimia 330 ambapo jumla ya wateja wapya 2,329 wamesajiliwa na kuunganishwa katika mtandao wa maji kati ya hao 1,436 Unguja na 893 Pemba.

Kwa upande wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), alisema shirika hilo limepanga kutumia Sh. bilioni 1.97 kwa kazi za usambazaji wa umeme katika vijiji 40, kwamba Unguja 22 na Pemba 18.

Hata hivyo alisema katika utekelezaji wa kazi hizo shirika limepeleka umeme katika vijiji 42 vilivyogharimu Sh. bilioni 1.98 sawa na asilimia 105.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MONICA JOSEPH MAKUNA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **P1189/0211** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BIAFRA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2005.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: KW/RB/587/2023**

## KUPOTELEWA NA CHETI



117264602

**LAWRENCE DASTAN MMBANDO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S0130/0031** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAUA SEMINARY** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/453307/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**LUGANO DANIEL MWANDAMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 634 CSB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/43518/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Ndugu CLEOPHACE LAURENT KABAKAMA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T177 ARF.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/50649/2023,** kwa yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0784299702.**

## TANGAZO KUPOTEA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

Hamisa Juma Omary ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu Asha Abzeti

Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 64 kitalu "DD" kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Hamisa Juma Omary kwa simu namba **0713-944171.**

**Taarifa ya polisi**
**SHI/SHI/RB/38824/2023.**

Jacob F. Mwinuka
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA
MUNICIPAL LAND OFFICER SHINYANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUBHASH NANJI PABARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 905 DND** aina ya **TOYOTA- WISH**, Chasis **No.ZNE100285044**, Engine **No.IZZ2464219**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya polisi
**MWA/NYA/RB/51030/2023**


## *OFISI ZA MATANGAZO*

***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042,***
***Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

# *Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Vifo vyafikia 5,000 tetemeko Uturuki, Syria

**ANKARA,** Uturuki

TAARIFA za mamlaka za serikali nchini Uturuki na Syria zimesema kuwa idadi ya waliofariki dunia imefikia watu 5,000, huku waokozi wakiendelea usiku kucha kuwatafuta watu walio chini ya kifusi.

Uturuki na Syria zilikumbwa na tetemeko kubwa la ardhi usiku wa kuamkia Jumatatu, na kusababisha vifo, uharibifu wa mali na miundombinu.

Shirika la Afya Duniani (WHO) lilikadiria kuwa huwenda waliokufa ni mara nane zaidi ya idadi inayojulikana hivi sasa.

Nchi mbalimbali zimepeleka vikosi vya kusaidia katika juhudi za uokozi, huku Shirika la Uturuki la kushughulikia majanga likisema zaidi ya wahudumu 24,400 wako katika maeneo yaliyoathirika.

Pia ilielezwa kuwa kutokana na ukubwa wa eneo lililopigwa na tetemeko hilo na kusababisha takribani nyumba 6,000 kuporomoka nchini Uturuki pekee, juhudi za wahudumu hao zinatajwa kuwa bado ni ndogo.

**Shirika la Afya Duniani (WHO) lilikadiria kuwa huwenda waliokufa ni mara nane zaidi ya idadi inayojulikana hivi sasa.**

Wizara ya Afya ya Uturuki ilisema kuwa magari ya kubebea wagonjwa yapatayo 813 yamepelekwa katika maeneo yaliyoathirika, yakiambatana na vikundi maalumu vya huduma za dharura zaidi ya 220.

Tetemeko lenye ukubwa wa 7.8 kwenye kipimo cha Richter liliitikisa sehemu ya katikati mwa Uturuki na kaskazini mwa Syria alfajiri ya juzi na kufuatiwa na jingine dakika 10 baadaye, likiharibu vibaya miundombinu katika miji ipatayo 12.

Inaelezwa kuwa kutokana na maafa makubwa yaliyotokana na tetemeko hilo nchini Uturuki na Syria, mataifa mbalimbali duniani yanafanya hima kupeleka misaada katika maeneo ya maafa.

Marekani inaratibu msaada wake katika shughuli za uokozi na kusambaza mahitaji ya kiutu.

Timu za uokozi za Russia kutoka wizara ya masuala ya dharura zilikuwa zikijiandaa kwenda Syria, kujiunga na vikundi vingine ambavyo tayari vinasaidia kuwatafuta watu chini ya kifusi.

Vile vile imebainishwa kuwa Umoja wa Ulaya (EU) unatumia mfumo wake wa satelaiti kuchora ramani za operesheni za uokozi, huku mataifa 13 wanachama yakiahidi msaada wa kiutu kwa Uturuki na Syria.

Pia inaelezwa kuwa tayari madaktari na wataalamu wa uokozi wa Ujerumani wameshaelekea Uturuki.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Ujerumani, ilisema nchi hiyo inaratibu msaada wake chini ya EU, ikiweka tayari shehena ya majenereta, mahema, mablanketi na vifaa vya kusafisha maji na timu ya uokozi inayojumuisha madaktari na wataalamu wa uokozi iliondoka nchini Ujerumani jana kuelekea Uturuki.

Waziri Mkuu wa Ugiriki, Kyriakos Mitsotakis, ambaye nchi yake imekuwa katika mgogoro wa muda mrefu na Uturuki kutokana na masuala ya mipaka na kitamaduni ameahidi pia msaada kwa taifa hilo jirani.

Kwa upande wake, Kamishna Mkuu wa Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa, Filipo Grand, ametoa wito wa mshikamano kwa Uturuki na Syria na kuongeza kwamba umoja huo uko tayari kutoa msaada wa haraka kwa waathirika.

Uturuki ni miongoni mwa nchi ambazo zimekuwa zikikumbwa na matetemeko ya ardhi mara kwa mara na kwamba mwaka 1999 watu 17,000 waliuawa kutokana na tetemeko la ardhi lenye ukubwa wa 7.6 katika kipimo cha Ritcha lilipoupiga mji wa Izmit na mwaka 2011 tetemeko jingine liliukumba mji wa Van na kusababisha vifo vya watu 500. **DW**



Mwonekano wa vifusi vya nyumba zilizoporomoka baada ya kukumbwa na tetemeko la ardhi nchini Uturuki juzi.
**PICHA: DW**

## Mahujaji 15 wa Nigeria wauawa Burkina

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

OFISI ya Rais wa Nigeria imesema takribani mahujaji 15 wakiislamu raia wa Nigeria waliokuwa wanaelekea Senegal wameuawa wakati watu wenye silaha nchini Burkina Faso walipolishambulia basi lililokuwa likiwasafirisha.

Msemaji wa ofisi ya Rais wa Nigeria aliiambia Reuters kupitia ujumbe wa WhatsApp jana kwamba idadi ya waliokufa ni 15 kufikia sasa.

"Rais Muhammadu Buhari amepokea taarifa za kusikitisha za mauaji hayo," alisema.

Aidha, kwa mujibu wa mamlaka ya kidini ya Senegal, washambuliaji wasiojulikana waliushambulia msafara wa mabasi Jumatano wiki iliyopita na kuua abiria 18.

Mahujaji hao walikuwa njiani kuelekea kwenye hafla ya kidini nchini Senegal, wakitokea Niger na Nigeria, safari ambayo inalazimu kuvuka ngome za wanamgambo wa kiislamu kaskazini mwa Burkina Faso na katikati mwa Mali. **VOA**



## Wananchi walicharukia jeshi la kikanda DRC

**KINSHASA,** DRC

MAMIA ya wananchi wamejitokeza barabarani kwa siku ya pili mjini Goma, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wakilishutumu Jeshi la Umoja wa Mataifa (UN) na Kanda ya Afrika Mashariki kwa kushindwa kuunga mkono operesheni za kijeshi za Kongo dhidi ya kundi la waasi la M23.

Inaelezwa kuwa takriban watu wawili walifariki Jumatatu kutokana na makabiliano makali kati ya waandamanaji hao na vikosi vya usalama vya DRC.

Kwa mujibu wa BBC, mapigano hayo yameongezeka katika eneo hilo kwa siku za hivi karibuni huku kundi hilo likichukua miji muhimu mashariki mwa DRC.

Pia inaelezwa kuwa baada ya maandamano hayo kuanza juzi vikosi vya usalama vilifyatua vitoa machozi kutawanya umati wa watu waliorusha mawe na mabomu ya petroli kwenye makao makuu ya UN huko Goma.

Waandamanaji hao wanadai kuwa walinda amani wa UN na Wanajeshi wa Kanda ya Afrika Mashariki wameshindwa kutoa msaada katika uwanja wa vita kwa Jeshi la Kongo katika kukabiliana na kundi la waasi la M23.

Aidha, inabainishwa kuwa waasi wameteka maeneo makubwa ya Mkoa wa Kivu Kaskazini wenye hali tete katika siku za hivi karibuni na wametishia kuandamana hadi Goma, eneo ambalo ni kitovu cha kibiashara.

Mapigano ya hivi majuzi yamesababisha vifo vya mamia ya watu na maelfu ya wengine kuyahama makazi yao. **BBC**

## Guterres ahofia kuenea vita Ukraine

**NEW YORK,** Marekani

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres, ameelezea hofu yake, kwamba vita vya Ukraine vinaweza kusambaa zaidi, huku akionya kuwa fursa ya kupata amani inafifia.

Guterres aliyasema hayo wakati akilihutubia Baraza Kuu la UN mjini New York, siku chache kabla ya kutimia mwaka mmoja tangu Russia ilipoanzisha vita dhidi ya Ukraine.

Katibu mkuu huyo alisema vita hivyo vimesababisha mateso yasiyosemeka kwa watu wa Ukraine na vinaambatana na athari kubwa kwa dunia nzima.

"Dunia inaelekea katika vita vipana bila kujitambua, huku umwagaji wa damu ukizidi kuongezeka," alisema Guterres.

Pia Guterres, alikemea vitisho vya kutumia silaha za maangamizi, akisema kinachozungumzwa na Russia kuhusu matumizi ya nyuklia ya kimkakati hakiingii akilini.

Kiongozi huyo alitahadharisha kwamba hatari kubwa ya kinyuklia inaweza kutokea kwa makusudi au kwa ajali. **DW**

# NBC DODOMA INTERNATIONAL MARATHON KUFANYIKA JULAI

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imetangaza msimu wa nne wa mbio za NBC Dodoma International Marathon 2023 zinazotarajiwa kufanyika Julai 23, mwaka huu katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, huku ikijivunia mafanikio makubwa yaliyotokana na mbio hizo ikiwamo kufanikiwa kukusanya fedha zaidi ya Sh. milioni 500 ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake (Cervical cancer).

Hafla ya uzinduzi wa mbio hizo ilifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa mchezo wa riadha nchini pamoja na wadau wa mbio hizo akiwamo Mwenyekiti wa Chama cha Riadha Tanzania (RT), William Kallaghe, Mkurugenzi wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Crispin Kahesa, wafanyakazi wa Benki ya NBC wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wao, Theobald Sabi pamoja na wadau wa vyombo vya habari.

**Akizungumza kwenye hafla hiyo, Sabi alisema kupitia uratibu wa mbio hizo katika kipindi cha miaka mitatu sasa, Benki ya NBC imefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. milioni 500 ambazo zilikabidhiwa kwa taasisi ya Saratani ya Ocean Road ili kufadhili upimaji na matibabu ya saratani hiyo kwa wanawake.**

"Ninayo furaha kuwajulisha kuwa ripoti ambayo wenzetu wa Ocean Road wametupatia, inaonyesha kuwa fedha zilizokusanywa kupitia mbio hizi, zimewezesha upimaji wa zaidi ya wanawake 20,473 ambapo kati yao 1,330 waligundulika kuwa na vimelea vya saratani ya shingo ya kizazi na wanaendelea na matibabu na wauguzi 98 wamepata mafunzo ya kusaidia wagonjwa wa saratani. Hili ni jambo kubwa na la kujivunia sana," alisema Sabi huku akiwapongeza washiriki na wadau wa mbio hizo kwa mafanikio hayo.

Aidha, Sabi aliongeza kuwa mbali na mafanikio hayo mbio hizo pia zimefanikiwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza utalii wa ndani na kufungua fursa za kiuchumi hususan katika Jiji la Dodoma ambapo zimekuwa zikifanyika.

Kwa upande wa Dk. Kahesa, alisema NBC imekuwa mdau mkubwa katika kupambana na saratani haswa ya shingo ya kizazi na kwamba takwimu zinaonyesha kati ya kesi 40,000 za saratani Tanzania, 26,000 ni saratani ya shingo ya kizazi.

"Matibabu ya saratani nayo ni gharama, kwani mgonjwa hulazimika kutumia kati ya milioni 10 hadi 40 katika matibabu. Kwa takwimu hizi zilizotolewa leo ni dhahiri kwamba NBC Dodoma Marathon inasaidia sana katika kuboresha afya na maisha ya Watanzania na kuwaondoloea jukumu kubwa la matibabu kwa sababu wanawake wanapopimwa mapema na kugundulika na vimelea hupatiwa matibabu ya awali kuzuia usambaaji wa saratani hii," alisema.

Mwenyeki wa RT, Kallaghe alisema: "NBC Dodoma Marathon ni kati ya mbio zenye viwango vya hali ya juu na vyenye mchango mkubwa katika kukuza mchezo huu wa riadha Tanzania. Tumeshuhudia wenyewe kuwa NBC Dodoma Marathon ni kati ya wadau wanaotoa zawadi kubwa kwa washindi ili kuleta hamasa na mwamko wa mchezo huu ndani na nje ya nchi.

"Naambiwa mwaka jana peke yake NBC Marathon ilivutia zaidi ya wanariadha wa kulipwa 60 kutoka mataifa mbali mbali," alisema.

Tangu kuanza kwa mbio hizo zinazoingia msimu wa nne mwaka huu zimekuwa zikibeba agenda ya kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake nchini. Aina hiyo ya saratani ndio inayoongoza kwa kuchangia vifo vingi zaidi vya wanawake Tanzania na katika nchi zinazoendelea.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akijipongeza sambamba na wadau wengine wa NBC Dodoma International Marathon katika uzinduzi wa mbio hizo uliofanyika Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Crispin Kahesa (kulia), Mwenyekiti wa Chama cha Riadha Tanzania (RT), William Kallaghe (wa pili kulia), Mkurugenzi wa Wateja Wadogo wa NBC, Elibariki Masuke (wa tatu kulia), Mkuu wa Kitengo cha Compliance Benki ya NBC, Sarah Laiser (wa pili kushoto) na Mkuu wa Uendeshaji wa EFM Radio na TVE, Dennis Ssebo, ( wa tatu kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

# Azam FC sasa yaipa kiburi Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Azam FC Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, Klabu ya Dodoma Jiji FC, imetamba kuwa gari limewaka na lengo lao ni kuchukua pointi tatu au moja kwenye kila mchezo uliopo mbele yao ili kujiweka sehemu salama katika msimamo wa Ligi Kuu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Kassim Liogope na Ofisa Habari wa klabu hiyo, Moses Mpunga, walisema baada ya kuifunga Azam, basi wanaamini hakuna kitakachoshindikana kama wakiwa na dhamira ya dhati ya kufanya hivyo.

"Kwa sasa tuko kwenye maandalizi makali kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar, lengo letu ni kwamba kila mechi inayokuja ni kupata pointi tatu, ikikosekana sana moja kwa sababu hali ilipofikia pointi moja tu inaweza kukusogeza mbali sana.

"Kabla ya kuifunga Azam tulikuwa nafasi ya 13, baada ya kushinda tumeenda moja kwa moja hadi nafasi ya 10, lakini Mbeya City ametushusha hadi nafasi ya 11 kwa mabao ya kufunga, wote tuna pointi 24," alisema Liogope.

Mpunga alisema kuwa baada ya kuitwanga Azam gari limewaka na haitoacha pointi kwenye michezo ambayo imesalia.

"Baada ya kuifunga Azam kila mmoja, kuanzia viongozi, wachezaji, benchi la ufundi, tumekuwa na ari kubwa, lengo letu ni lilelile kubaki Ligi Kuu, tunataka mpaka ligi inaisha tuwe moja ya timu ambazo hazitoshuka daraja, wala kwenda kucheza mechi za mchujo na hilo linawezekana kabisa," alisema.

Timu hiyo imecheza mechi 22, ikishinda saba, sare tatu na kupoteza 12 huku ikiwa na mabao 16 ya kufunga na kuruhusu 27.

# Mwaisabula: Musonda bado Yanga

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Kenny Mwaisabula, amemfuatilia kwa kina mshambuliaji mpya wa Yanga, Kennedy Musonda raia wa Zambia, katika michezo aliyoichezea timu hiyo na kusema "bado ana kazi kubwa ya 'kukopu' mfumo wa timu hiyo" kwa kuwa muda ni mdogo kuweza kuwa sawa.

Yanga ilimsajili Musonda katika usajili wa dirisha dogo uliofungwa Januari 15, mwaka huu kwa lengo la kusaidiana na kinara wa mabao wa timu hiyo, Fiston Mayele, ili kuleta ushindani katika Ligi Kuu Bara na mechi za Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga inayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, itashuku dimbani ugenini nchini Tunisia Jumapili wiki hii kuwavaa wenyeji wao, Us Monastir katika mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwaisabula alisema kuwa, mara nyingi usajili wa dirisha dogo wachezaji wamekuwa na ugumu kidogo kuweza kwenda na mfumo tofauti na dirisha kubwa, hivyo itampa wakati mgumu Musonda kuweza kuelewana na Mayele kwa haraka.

"Musonda anaweza kusaidiana na Mayele, lakini dirisha dogo wachezaji 'kukopu' inachukua muda kidogo tofauti na dirisha kubwa watu wanakuwa katika kipindi cha preseason hivyo wanajiandaa na timu tofauti na sasa.

"Mchezaji kukopu anachukua muda, inakuwa rahisi kwa mchezaji ambaye amecheza ligi hii kama vile Saido (Ntibazonkiza), imekuwa rahisi kutokana na kuijua ligi ya hapa tofauti na mchezaji kutoka nje ya ligi hii," alisema na kuongeza:

"Mchezaji kutoka nje pia itamchukua muda kuweza kumzoea mwalimu, wachezaji na hata mazingira aliyoyakuta, hivyo itamchukua muda kidogo Musonda kwenda sawa na Mayele."

Aidha, akizungumzia kuhusu Bernard Morrison kuwa nje kwa miezi miwili kutokana na majeruhi ya nyonga, hivyo kushindwa kuichezea Yanga mechi za kimataifa, Mwaisabula alisema: "Litakuwa ni pengo kukosekana kwa Morrison katika michuano ya kimataifa kwa kuwa ni mchezaji wa kimataifa na ana uzoefu wa mechi za kimataifa hivyo angeisaidia timu.

"Lakini naamini Yanga itafanya vizuri kwa kuwa ina wachezaji wazuri wa kimataifa kama Aziz Ki na Mayele."

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SILVA ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inataka kumsajili kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva, mwenye umri wa miaka 28, ambaye yuko tayari kuondoka Manchester City, lakini inaweza kukabiliana na ushindani kutoka kwa Barcelona. ***(Le10 Sport)***

### UNITED KUMUUZA MARTIAL

KLABU ya Manchester United itajaribu kuwauza Anthony Martial mwenye umri wa miaka 27, beki wa kati wa England, Harry Maguire mwenye miaka 29 na beki wa kushoto wa Brazil, Alex Telles mwenye miaka 30 katika msimu wa majira ya joto huku klabu hiyo ikilenga kutoa nafasi kwa mshambuliaji mpya kutoka Klabu ya Tottenham nahodha, Harry Kane, 29, au mchezaji wa kimataifa wa Napoli, Victor Osimhen, 24. ***(Mail)***

### SPURS YAMKOMALIA KANE

TOTTENHM Hotspur imesema haitamuuza mfungaji wake bora wa klabu, Harry Kane, 29, kwa klabu pinzani msimu huu wa majira ya joto. ***(Times)***

### RICE ATAJWA UNITED

MANCHESTER United itahitajika kulipa pauni milioni 120 kumnunua kiungo wa kati wa England, Declan Rice, 24, kutoka West Ham, baada ya dau la pauni milioni 100 kukataliwa msimu uliopita. ***(TalkSport)***

### CARBERAN KUINOA LEEDS

CARLOS Corberan wa West Brom anaongoza kwenye orodha fupi ya Leeds United ya kocha wa kuchukua nafasi ya Jesse Marsch aliyetimuliwa. ***(Guardian)***

### JUDE NA REAL MADRID

REAL Madrid inaamini kuwa kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, 19, atachagua kuhamia Ligi Kuu England atakapoondoka Borussia Dortmund. ***(Athletic)***

### JONES NA SOUTHAMPTON

WAMILIKI wa Klabu ya Southampton walijadili mustakabali wa kocha, Nathan Jones baada ya timu hiyo kuchapwa mabao 3-0 Jumamosi na Brentford, lakini wanatazamiwa kuendelea kubaki naye kwa sasa. ***(Sport)***

### ANUKIA HOFFENHEIM

KOCHA wa zamani wa Southampton, Ralph Hasenhuttl, anaongoza mbio za kuwa kocha mpya wa klabu ya Ujerumani ya Hoffenheim baada ya kutimuwa Andre Breitenreiter. ***(Sky Sports)***

### COSTA AFUATILIWA CHELSEA

CHELSEA inamfuatilia mlinda mlango wa Porto na Ureno, Diogo Costa, 23, huku wakitarajia kushughulikia mustakabali wa mlinda mlango wao katika majira ya joto. ***(90Min)***

### ADARABIOYO AWINDWA INTER

INTER Milan wamemwongeza mlinzi wa Fulham, Tosin Adarabioyo, 25, kwenye orodha ya nyota inayowasaka kuchukua nafasi ya mlinzi wa kati wa Slovakia, Milan Skriniar, 27, ambaye anatarajiwa kuondoka katika kikosi hicho cha Serie A mkataba wake utakapokamilika msimu wa majira ya joto. ***(Tuttomercatoweb)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND SASA AKOSOLEWA UAMUZI KUJIUNGA MAN CITY

**●●● Uliona kasi yake, huenda alichagua klabu isiyo sahihi, hatuoni kila kitu chake...**

**LONDON,** England

JAMIE Carragher amedai kwamba, Erling Haaland huenda alichagua klabu isiyo sahihi kwa kujiunga na Manchester City.

**Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Norway anaongoza kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu England msimu huu akiwa na mabao 25 katika mechi 20.**

Katika kipigo cha juzi cha bao 1-0 kutoka kwa Tottenham Hotspur, Haaland hakuwa na mguso hata mmoja kuelekea timu pinzani ikiwa ni mara ya kwanza katika msimu wake wa kwanza nchini England.

Kipigo cha City kiliwafanya vijana wa Kocha Pep Guardiola kukosa nafasi ya kupunguza uongozi wa Arsenal kileleni kwenye msimamo hadi pointi mbili pekee na wanakaa pointi tatu pekee mbele ya majirani zao Manchester United.

Imependekezwa City ni timu dhaifu huku Haaland akiwa upande wake, lakini Carragher aliienda mbali zaidi kwa kudai kuwa mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund huenda alijiunga na upande usiofaa kwa mahitaji yake.

"Najua hilo halipo kila wakati kutokana na jinsi City wanavyocheza. Ametoka kwenye ligi ya mashambulizi ya kaunta (Bundesliga)," alisema Carragher akiiambia Daily Mail.

"Uliona kasi yake, huenda alichagua klabu isiyo sahihi ili kupata matokeo bora zaidi kutoka kwake.

"Hatuoni kila kitu cha Haaland. City wamefunga idadi kamili ya mabao kama msimu uliopita. Amefunga mabao 25, lakini City kwa ujumla wamefunga idadi sawa kwa jumla. Hata hivyo, wameruhusu zaidi na ni rahisi kushambulia dhidi yao hivi sasa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,074,7

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 08,09 NA 10 FEBRUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/02/23 | 20:00 | Nurnberg vs Fortuna Dusseldorf | 2.64 | 3.34 | 2.62 |
| 02. 08/02/23 | 20:15 | Angers vs Nantes | 2.35 | 3.18 | 2.98 |
| 03. 08/02/23 | 20:15 | Toulouse vs Reims | 2.35 | 3.29 | 2.89 |
| 04. 09/02/23 | 01:30 | Bragantino SP vs Sao Paulo | 2.65 | 3.06 | 2.53 |
| 05. 09/02/23 | 02:30 | Botafogo SP vs Ituano SP | 2.52 | 2.95 | 2.74 |
| 06. 09/02/23 | 03:00 | Nacional Potosi vs El Nacional Quito | 2.21 | 3.29 | 2.91 |
| 07. 09/02/23 | 04:05 | Pumas De Tabasco vs Correcaminos Uat | 2.35 | 3.22 | 2.75 |
| 08. 09/02/23 | 11:30 | Aizawl FC vs Rajasthan United | 2.48 | 2.95 | 2.80 |
| 09. 09/02/23 | 14:00 | Gokulam Kerala FC vs Minerva FC | 2.57 | 3.01 | 2.64 |
| 10. 09/02/23 | 20:00 | Nea Salamis vs Anorthosis Famagusta | 2.63 | 3.04 | 2.77 |
| 11.10/02/23 | 00:00 | Santo Andre SP vs EC Agua Santa SP | 2.30 | 2.90 | 3.11 |
| 12.10/02/23 | 04:05 | Queretaro FC vs Club Leon | 2.60 | 3.55 | 2.45 |
| 13.10/02/23 | 11:45 | Brisbane Roar vs Central Coast Mariners | 2.81 | 3.24 | 2.43 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa


SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE GEA AAMINI SABITZER ATAZIBA PENGO LA CASEMIRO



**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea amesema itakuwa vigumu kucheza mechi tatu za Ligi Kuu England bila uwapo wa Casemiro, lakini anaamini kiungo Marcel Sabitzer atavaa viatu vya kiungo huyo vizuri kabisa.

Kiungo Casemiro alitolewa kwa kadi nyekundu katika mchezo wa Ligi Kuu England mwishoni mwa wiki dhidi ya Crystal Palace, ambapo Man United ilishinda kwa mabao 2-1 na hivyo mchezaji huyo atakosa michezo mitatu ya ligi ijayo ya klabu hiyo.

De Gea anaamini usajili mpya ndani ya klabu hiyo kutoka Bayern Munich, Sabitzer, anaweza kuziba pengo la Casemiro, kwani mchezaji huyo ana uzoefu na ameshacheza michezo mingi kwenye Ligi ya Ujerumani hivyo anaweza kuwasaidia.

Golikipa huyo alikataa kuzungumzia tukio la Casemiro la kupewa kadi nyekundu na mwamuzi wa mchezo huo, kwani alisema hataki kuzungumza kwa kuwa inaweza kumweka kwenye matatizo.

Casemiro alipewa kadi nyekundu ya moja kwa moja kwa mara ya kwanza katika michezo yake 366 aliyoitumikia klabu ya Real Madrid pamoja na Man United. Hiyo ni kutokana na kuonekana kufanya kitendo ambacho si cha kiungwana michezoni.



## Hazard pancha tena Madrid

**MADRID,** Hispania

WINGA wa Real Madrid, Eden Hazard, amepata jeraha lingine linalomfanya kukaa nje ya uwanja kwa muda usiojulikana.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ameumia kwenye goti lake la kushoto, ikiwa ni mara yake ya 18 kurejea katika klabu hiyo tangu ajiunge na wababe hao wa Hispania kutoka Chelsea msimu wa majira ya joto wa 2019.

Hazard ambaye ni majeruhi, amecheza mechi tatu pekee za ligi msimu huu, na mchezaji huyo aliyenunuliwa kwa pauni milioni 150, anatarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa mara nyingine tena.

Real Madrid ilisema katika taarifa yake: "Baada ya vipimo vilivyofanywa leo (juzi) Eden Hazard amegundulika kuwa ameumia goti lake la kushoto na yuko chini ya uangalizi."

Hazard amecheza mechi tatu pekee za Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu hadi sasa msimu huu, akiwa ameanza mara moja tu, na hajacheza kabisa kwenye ligi tangu Septemba 9, mwaka jana dhidi ya Real Mallorca.

Katika mashinda yote ya msimu huu, am cheza dakika 296 pek katika mechi 7 na alian mara tatu pekee dhidi Mallorca, Celtic kwen Ligi ya Mabingwa Ula na Cacereno ya Dara la Nne kwenye Copa d Rey.

Mchezaji huyo kimataifa wa Ubelg mwenye mechi 126, a chukuliwa kuwa mmo wa wachezaji bora za duniani alipoondo Chelsea mwaka wa 20 kwa mkataba wa thama ya hadi pauni milioni 15

741,067/-

# BETIKA YAZINDUA MTOKO WA KIBINGWA KARIAKOO 'DABI'

**Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa soka 100 wa Simba na Yanga watashuhudia kibingwa mechi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu itakayochezwa Aprili 16, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Mashabiki hao ni wale watakaoibuka washindi kwenye 'Droo ya Betika Mtoko wa Kibingwa' iliyozinduliwa jana katika Hoteli ya Serena, Dar es Salaam.**

Akizungumza katika uzinduzi huo jana, Meneja Mkuu wa Betika Tanzania, Tumaini Maligana, alisema washindi 10 wa droo ya kwanza watatangazwa ifikapo Februari 13, mwaka huu.

"Droo itafanyika kila wiki na kutoa washindi zaidi ya 10 na tamati itakuwa ni wiki ya mwisho ya siku ya dabi," alisema Maligana na kuongeza:

"Ni rahisi kushinda, ambapo mshiriki anaweza kuweka bashiri zake katika ligi mbalimbali ikiwamo ya EPL, LaLiga, Bundesliga, Serie A na Ligi ya Bongo ikiwamo mechi ya Simba na Yanga."

Alisema huu ni msimu wa tano wa Droo ya Mtoko wa Kibingwa ambapo washindi 400 wamepata fursa ya kushuhudia dabi hiyo kwa gharama za Betika.

"Kwenye dabi iliyopita tulipata washindi 50 ambao walikuja kushuhudia mechi hiyo ya watani wa jadi 'Ki-VIP', msimu huu 'tumedabo' na mashabiki 100 kutoka maeneo mbalimbali nchini wana fursa ya kushinda," alisema.

Alisema yeyote atakayejisajili na Betika atakuwa ameingia moja kwa moja kwenye Mtoko wa Kibingwa.

"Atakayecheza pia beti tano za kuanzia Sh. 500 au zaidi ataingia katika Droo ya Mtoko wa Kibingwa moja kwa moja bila kujali mkeka umetiki au la!.

"Washindi kutoka nje ya Dar es Salaam watasafiri kwa ndege na kutakuwa na 'pati' kabla ya dabi hiyo, kisha tukio la Mtoko wa Kibingwa litakalokwenda sanjari na uchambuzi wa mechi ya dabi na matukio mengine mbalimbali.

"Siku ya mechi wataongozwa na king'ora kwenda kwa Mkapa kushuhudia dabi hiyo na baada ya mechi washindi hawatarudi mikono mitupu, wataondoka na zawadi mbalimbali," alisema.




Msanii wa Muziki wa RNB nchini, Juma Mussa Mkambala maarufu Jux, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu mafanikio ya ziara yake jijini Paris, Ufaransa, iliyoandaliwa na Cognac yenye mafunzo mbalimbali kuhusu Chapa ya Hennessy na mpira wa kikapu, ambapo alitembelea uwanja mkongwe zaidi wa mpira huo wa Trevise Court. **PICHA: JOHN BADI**

## Simba: Tumeisoma

INATOKA UKURASA 24

wa ugenini kabla ya kurejea nyumbani kwa ajili ya kutafuta pointi tatu za nyumbani," alisema Mgunda.

Alisema malengo yao muhimu ni kutafuta pointi tatu kila mechi, nyumbani na alama zote tatu ugenini, lakini wakikosa basi angalau warejee na pointi moja wakianza na mchezo dhidi ya Horoya AC.

Kuelekea michezo yao ya kimataifa, uongozi wa Simba jana usiku walitambulisha rasmi jezi ambazo watakazotumia katika michuano hiyo.

## *Yanga yaanika njia*

INATOKA UKURASA 24

shaanza kuuza tiketi za mchezo huo huku kiwango cha juu kikiwa ni Sh. 20,000 kwa VIP A, B 15,000, C , 10,000 na 3,000 kwa mzunguko kuanzia leo na 5,000 zitauzwa kwa wanaonunua siku ya mchezo.

"Katika mchezo huo dhidi ya TP Mazembe, utakuwa ni mechi yetu ya kwanza ya hatua ya makundi hapa nyumbani ya Kombe la Shirikisho, tumeipa uzito wake na kuipa jina maalum la 'Wananchi Super Sunday'," alisema Kamwe.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/02/23 | 18:00 | Southampton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 02. 11/02/23 | 18:00 | KVC Westerlo vs KAA Gent | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 11/02/23 | 18:15 | UD Almeria vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.30 | 2.44 |
| 04. 11/02/23 | 22:45 | Lazio Rome vs Atalanta BC | 2.27 | 3.35 | 3.00 |
| 05. 11/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Athletic Bilbao | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 06. 12/02/23 | 09:00 | Macarthur FC vs Wellington Phoenix FC | 2.55 | 3.15 | 2.29 |
| 07. 12/02/23 | 15:00 | Toulouse FC vs Stade Rennes | 3.05 | 3.35 | 2.25 |
| 08. 12/02/23 | 16:00 | Getafe CF vs Rayo Vallecano | 2.75 | 2.85 | 2.80 |
| 09. 12/02/23 | 16:30 | Vitesse Arnhem vs FC Utrecht | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 12/02/23 | 17:00 | Angers SCO vs AJ Auxerre | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 12/02/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs Stade Brest 29 | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 12. 12/02/23 | 17:30 | Hertha BSC vs Borussia Monchengladbach | 2.75 | 3.50 | 2.37 |
| 13. 12/02/23 | 18:15 | RC Celta de Vigo vs Atletico Madrid | 3.40 | 3.05 | 2.24 |
| 14. 12/02/23 | 19:30 | 1. FC Cologne vs Eintracht Frankfurt | 2.65 | 3.45 | 2.47 |
| 15. 12/02/23 | 20:30 | Real Valladolid vs CA Osasuna | 2.60 | 3.05 | 2.80 |
| 16. 12/02/23 | 21:00 | Sporting Lisbon vs FC Porto | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 17. 12/02/23 | 22:45 | Olympique Lyon vs RC Lens | 2.39 | 3.40 | 2.80 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 08/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3976 | Nairobi City Stars FC vs Kenya Police | 4.36 | 2.96 | 1.88 |
| 13:30 | 3279 | HJK Helsinki vs Lahti | 1.29 | 4.86 | 8.27 |
| 13:30 | 3609 | Havadar vs Teraktor Sazi | 3.11 | 2.56 | 2.58 |
| 14:00 | 3549 | Neroca FC vs Kenkre FC | 1.63 | 3.74 | 4.57 |
| 14:30 | 5354 | A.C Milan W vs Fiorentina W | 1.55 | 3.90 | 4.20 |
| 15:00 | 2134 | Monori SE vs Paksi FC | 10.17 | 5.40 | 1.22 |
| 15:00 | 2175 | Ivancsa Kse vs Budafoki Mte | 2.85 | 3.32 | 2.23 |
| 15:00 | 5253 | Esmtk Budapest vs Kisvarda FC | 10.17 | 5.40 | 1.22 |
| 15:15 | 2648 | Ho Chi Minh City vs Hai Phong | 3.05 | 3.21 | 2.17 |
| 16:00 | 1650 | Esperance Tunis vs ES Hammam Sousse | 1.43 | 3.56 | 8.47 |
| 16:00 | 2042 | AL Akhdood vs AL Riyadh | 2.70 | 2.85 | 2.64 |
| 16:00 | 2857 | EO Sidi Bouzid vs ES Metlaoui | 2.22 | 2.57 | 3.84 |
| 16:00 | 3292 | Avenir Rjich vs US Monastir | 6.42 | 2.85 | 1.69 |
| 16:00 | 3492 | ES Sahel vs Club A Bizertin | 1.38 | 3.89 | 8.50 |
| 16:00 | 3546 | Al Orubah vs Al Qadisiyah | 2.74 | 2.74 | 2.69 |
| 16:00 | 3550 | Stade Tunisien vs US Tataouine | 1.78 | 2.83 | 5.36 |
| 16:00 | 3986 | Fiorentina Youth vs Atalanta Youth | 2.20 | 3.15 | 3.05 |
| 16:00 | 4871 | US Ben Guerdane vs AS Slimane | 2.13 | 2.64 | 3.98 |
| 16:00 | 5172 | CS Sfaxien vs CS Chebba | 1.81 | 2.81 | 5.20 |
| 16:00 | 5741 | Olympique de Beja vs Africain | 2.85 | 2.48 | 2.90 |
| 16:10 | 3554 | Ohud Medina vs Al Jabalain | 2.64 | 2.85 | 2.70 |
| 16:40 | 1545 | Al Salmiyah vs Al Fehaheel | 2.04 | 3.26 | 3.31 |
| 17:00 | 1668 | USM Alger vs RC Arbaa | 1.51 | 3.79 | 5.81 |
| 17:00 | 2047 | East Bengal vs Northeast United FC | 1.68 | 3.89 | 4.04 |
| 17:45 | 1161 | Sitra Club vs Muharraq SC | 5.08 | 3.42 | 1.64 |
| 17:45 | 2349 | Riffa Club vs Bahrain Club | 1.37 | 4.25 | 7.46 |
| 19:10 | 4034 | Al Kuwait SC vs AL Sahel | 1.26 | 4.70 | 7.40 |
| 20:00 | 1560 | Pafos FC vs AEL Limassol | 1.58 | 3.78 | 5.74 |
| 20:00 | 2658 | Nurnberg vs Fortuna Dusseldorf | 2.64 | 3.34 | 2.62 |
| 20:00 | 4221 | AD Grecia vs Guadelupe FC | 2.17 | 3.26 | 3.00 |
| 20:15 | 1059 | Lyon vs Lille | 2.09 | 3.43 | 3.28 |
| 20:15 | 1232 | Toulouse vs Reims | 2.35 | 3.29 | 2.89 |
| 20:15 | 1340 | Paris FC vs Annecy FC | 2.02 | 3.28 | 3.63 |
| 20:15 | 2207 | AJ Auxerre vs Rodez Aveyron | 1.60 | 3.78 | 5.37 |
| 20:15 | 3627 | Vierzon FC vs Grenoble Foot | 4.89 | 3.84 | 1.64 |
| 20:15 | 4408 | Angers vs Nantes | 2.44 | 3.19 | 2.84 |
| 20:45 | 5475 | PSV Eindhoven vs Emmen | 1.24 | 5.37 | 9.30 |
| 21:00 | 5163 | FC Gyori Eto vs Debreceni VSC | 3.16 | 3.32 | 2.07 |
| 21:45 | 4716 | Famalicao vs Belenenses | 1.45 | 3.99 | 6.22 |
| 22:00 | 2628 | Al Ahly Cairo vs Real Madrid | 8.08 | 4.76 | 1.30 |
| 22:00 | 5723 | SV Spakenburg vs VV Katwijk | 3.01 | 3.42 | 2.10 |
| 22:30 | 1674 | FC Winterthur vs Servette Geneva | 3.07 | 3.34 | 2.22 |
| 22:45 | 1343 | Sunderland vs Fulham | 3.85 | 3.65 | 1.81 |
| 22:45 | 3593 | VfL Bochum vs Borussia Dortmund | 4.24 | 3.91 | 1.76 |
| 22:45 | 3866 | Dundee FC vs Raith Rovers | 1.84 | 3.48 | 3.74 |
| 22:45 | 4612 | Gosport Borough vs Weston Super Mare | 2.96 | 3.74 | 2.02 |
| 23:00 | 1290 | Feyenoord vs NEC Nijmegen | 1.35 | 4.76 | 6.83 |
| 23:00 | 2326 | Manchester Utd vs Leeds | 1.48 | 4.29 | 5.78 |
| 23:10 | 2805 | Marseille vs Paris St Germain | 2.95 | 3.44 | 2.25 |
| 23:45 | 2453 | Viseu vs Porto | 9.11 | 5.39 | 1.24 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Februari 8, 2023
Nipashe



Haaland akosolewa kujiunga Man City

UKURASA 21

# Yanga yaanika njia kuvuka makundi CAF

●●● Yatua Tunisia na bunduki zote ikiitaja TP Mazembe, yasema hesabu zote kwa Mkapa...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kwenda nchini Tunisia ikihitaji angalau pointi moja katika mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi wa Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga imetangaza itakavyomaliza hesabu zake na kutinga robo fainali ya michuano hiyo, ambapo imesema imewekeza nguvu kubwa michezo ya nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kuvuna pointi zote tisa.

**Yanga iliondoka jana mchana kwa Shirika la Ndege la Emirates hadi Dubai ambapo ilitarajiwa kufika saa 3:50 usiku na leo saa 2:40 asubuhi kuanza safari ya kuelekea jijini Tunis, Tunisia tayari kwa mchezo wao huo wa kimataifa dhidi ya US Monastir utakaopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Olympique de Rades nchini humo.**

Katika uwanja huo wa Olympique de Rades kwenye mechi za mchujo, ndipo Yanga ilipofanikiwa kutinga hatua ya makundi baada ya kuitoa Club Africain ya Tunisia kwa kuichapa bao 1-0 baada ya mechi ya mkondo wa kwanza iliyopigwa dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, timu hizo kutoka suluhu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema kikosi cha wachezaji 25 kimeondoka kuelekea jijini Tunis tayari kwa mchezo wao dhidi US Monastir, lengo likiwa ni kupata pointi tatu na kama wakishindwa kuvuna zote, basi wapate angalau alama moja.

"Kati ya wachezaji hao 25, kipa wetu Abdultalib Mshery naye yupo kwenye msafara huo kwa ajili ya kwenda nchini humo kufanyiwa matibabu ya jeraha la mguu linalomsumbua.

"Pia katika msafara huo kuna benchi la ufundi la watu tisa na viongozi tisa akiwamo Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Issa Bukuku, ambaye ni mkuu wa msafara," alisema Kamwe.

Alisema wamejiandaa vizuri katika mchezo huo, kwa kutambua umuhimu wa mechi hiyo na tayari Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, alishatangulia nchini humo kwa ajili ya kuweka mambo sawa.

"Licha kwamba tunaenda Tunis na kikosi imara kutafuta pointi muhimu dhidi ya US Monastir, lakini nguvu zetu kubwa tumezielekeza mchezo wetu wa nyumbani utakaopigwa Febuari 19, mwaka huu dhidi ya TP Mazembe ambao tutacheza nyumbani.

"Wanachama na mashabiki wa Yanga watambue kila mechi kwetu ni muhimu, tunaenda Tunisia kutafuta pointi na tusipoteze, lakini tunahitaji kupata matokeo mazuri katika michezo yetu mitatu ya nyumbani kwa kupata pointi tisa," alisema Kamwe.

Kamwe alisema kwa kutambua umuhimu wa mchezo wao dhidi ya TP Mazembe, wame-

INAENDELEA UKURASA 23



Mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, ambaye bao lake pekee dhidi ya Club Africain katika Uwanja wa Olympique de Rades nchini Tunisia lilipelekea timu yake hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, ni miongoni mwa nyota watakaoivaa US Monastir Jumapili wiki hii katika uwanja huo. **PICHA: MAKTABA**

## Simba SC: Tumeisoma Horoya AC

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, amesema tayari wamefanikiwa kuona ubora wa Horoya AC ulipo na udhaifu wao, hivyo wataenda nchini Guinea kikamilifu kwa ajili ya kusaka pointi muhimu katika mchezo huo wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba ambayo tayari imetanguliza watu wake nchini Guinea kwa ajili ya kuandaa mazingira mazuri ya timu itakaposhukia, jana usiku ilitarajia kutangaza tarehe rasmi ya kuelekea nchini humo kwenye mechi yao ya kwanza ya hatua ya makundi msimu huu ambayo itapigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa General Lansana Conte.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema wanafahamu wanaenda kucheza na aina gani ya timu na wameandaa kikosi cha timu yao vizuri kwa ajili ya kusaka matokeo chanya.

Alisema wanahitaji kupata matokeo mazuri, hivyo wamewataka washambuliaji kuwa makini kwa kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza kupata bao na kutoruhusu Horoya AC kufanya mashambulizi lango mwao.

"Tumeona ubora wa Horoya AC, wako vizuri, tunaenda kwa tahadhari kubwa, wachezaji wanatambua umuhimu wa mchezo huo ni kutafuta pointi, tunaendelea kuimarisha kikosi hususan safu ya ulinzi kuwa makini na washambuliaji wa timu pinzani.

"Wakati tukipambana wapinzani wasipate bao, tunahitaji kuwa makini kutafuta alama hata moja katika mchezo huo

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >